




**Kikongwe** wa miaka 80 jela miaka 20 kisa ngozi ya chui

UKURASA 18




UKURASA 11

Nipashe
Jumatatu Februari 20, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581227
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

RIPOTI MAALUM

# Kazi nyumbani kwa mwalimu zilivyo kichaka cha ukatili

• **Mwalimu** adaiwa kunajisi mwanafunzi aliyemwita kuosha vyombo, apata ujauzito... *Endelea ukurasa 4*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### SERIKALI KUUFUTA USAJILI SHULE ZILIZOFANYA UDANGANYIFU MTIHANI

SERIKALI imeagiza kufanyika uchunguzi wa kina kuhusu shule nne zilizofanya udanganyifu kwenye mtihani wa kidato...

UKURASA WA 7

### KAMPENI YA CRDB KUONGEZA UJUMUISHI HUDUMA ZA KIFEDHA

WAKAZI wa Moshi mkoani Kilimanjaro wameonekana kuipokea vyema...

## Mch. Kimaro ataja sababu za kupewa likizo siku 60 KKKT

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Waziri Mkuu wa Ethiopia, Dk. Abiy Ahmed, Makao Makuu ya Umoja wa Afrika (AU) Addis Ababa, Ethiopia jana. **PICHA: IKULU**



## Mauaji yatikisa, yamo ya mjamzito, mchimbaji

UK. 2

**MICHEZO** **YANGA SC, AZAM FC ZAIVURUGA KMC** UK.24

**KATUNI** UK.6

# Mauaji yatikisa, yamo ya mjamzito, mchimbaji

**Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Temeke, Dar es Salaam, Juma Matumbi (32) ameuawa kwa kupigwa na wananchi wenye hasira kwa madai ya kuchukizwa na kitendo cha kuwapiga nondo wakazi wawili wa Kitongoji cha Ligunga, Kata ya Ngongowele wilayani Liwale mkoani Lindi.

Watu waliodaiwa kushambuliwa na Mtumbi ni Maneno Mathias (30), Paul Makonda (sio aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam) na Amina Sango anayedaiwa kuwa mpenzi wa marehemu.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo ambao hawakutaka kutajwa majina yao, walisema tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki, baada ya wenyeji waliompokea kumpatia eneo aliloomba kuchimba madini kwa ajili ya ujenzi.

Walisema siku aliyopewa eneo, alirejea alikofikia na kupata viburudisho na muda mfupi alianza kufanya fujo ikiwamo kukamata kuku na kukata kichwa kwa kumng'ata kwa meno.

Mashuhuda hao walidai kitendo hicho kilimshangaza mpenzi wake na alipohoji, alimshushia kipigo, kilichomsukuma jirani yake Maneno Mathias (30) kuingilia kati.

Walidai kuwa wakati Mathias akijaribu kuamua mgogoro huo, Matumbi alichukua nondo na kumchoma tumboni na kupelekea kifo chake.

"Mathias baada ya kuchomwa na nondo tumboni alikimbia, lakini hakuwahi kufika alikokusudia na kuanguka chini na kufariki dunia," walidai mashuhuda hao.

Walisema kitendo cha Mathias kukimbia, Matumbi alimfuatilia baada ya kumkosa aliyemkusudia aliingia ndani ya nyumba anayoishi Makonda amejipumzisha, akamchoma nondo mgongoni, kiunoni na kumsababishia maumivu makali.

Mashuhuda hao walisema kitendo hicho kiliwachukiza wananchi ndipo walimshambulia kwa kutumia mawe na marungu na kufariki dunia.

Kamanda wa Polisi Mkoani Lindi, Pili Mande, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na watu hao kupoteza maisha huku mmoja akijeruhiwa.

Alisema Makonda amelazwa katika Hospitali ya Wilaya Liwale akiendelea na matibabu na kwamba hakuna anayeshikiliwa huku wakiendelea kuwasaka waliohusika.

**MJAMZITO AUAWA**

Wakati hayo yakiendelea Lindi, mkoani Geita vijana wawili wameuawa na wananchi wenye hasira kwenye Kitongoji cha Kilimahewa, Kata ya Ludete mkoani Geita baada ya kutekeleza mauaji ya mama mjamzito, Renatha Elias na kumjeruhi mume wake, Msafiri Renatus kwa kumchoma kisu sehemu mbalimbali ya mwili kisha kutaka kukimbia.

Inadaiwa kuwa mmoja wa vijana hao ni mwanafamilia na ni mtoto wa nje ambaye alifika na kijana mwenzake kwenye nyumba hiyo na kutekeleza mauaji ya mjamzito huyo wakati akiwa bafuni anaoga.

Mwenyekiti wa kitongoji hicho, Marco Chuma, alisema aliyeuawa ni mama wa mji, mkuu wa kaya naye alipofika kwa ajili ya kupambana nao, alijeruhiwa kwa kuchomwa kisu maeneo mbalimbali ya mwili na kukimbizwa hospitalini.

Mkuu wa Wilaya ya Geita, Cornel Mgembe, aliyetembelea familia hiyo, alikemea matukio ya mauaji huku akiliagiza Jeshi la Polisi kuchukua hatua kali dhidi ya waliohusika.

"Kama una kijana au ndugu yako ambaye unafikiri anaweza kuendelea kutenda ujinga wa namna hii, mkanye mapema, hatutasita kumchukulia hatua stahiki za kisheria," alionya.

***Imeandaliwa na Said Hamdani (LINDI) na Vitus Audax (GEITA)**




Wananchi wilayani Muheza mkoani Tanga wakiangalia gari la wagonjwa lililombeba Christina Ngusi anayedaiwa kuchomwa visu mwili mzima na mpenzi wake. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Wafanyakazi wa kujitolea warejea baada UVIKO-19

**Na Jenifer Gilla**

WAFANYAKAZI wa kujitolea kutoka Shirika la Peace Corps lenye makao makuu Marekani jana walirejea nchini baada ya kutokuwapo kwa takribani miaka mitatu tangu kuripotiwa mgonjwa wa kwanza wa UVIKO-19 Machi 2020.

Taarifa iliyotolewa jana na Ubalozi wa Marekani nchini, ilibainisha kuwa kundi la kwanza lenye wafanyakazi 18 liliwasili jana tangu kuzuka kwa janga hilo lililolazimisha kurejeshwa nyumbani zaidi ya wafanyakazi 7,000 kutoka maeneo mbalimbali duniani.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa kabla ya kurejeshwa nyumbani, wafanyakazi hao zaidi ya 3,200 walitoa huduma nchini kwa zaidi ya miongo sita kuanzia Septemba 1961 hadi Machi 2020, wakifanya kazi ya kushughulikia vipaumbele muhimu vya maendeleo, zikiwamo sekta za elimu, kilimo na afya na kukuza amani ya dunia na urafiki.

Mkurugenzi Mkazi wa Peace Corps Tanzania, Stephanie Joseph de Goes alisema kurejea kwa wafanyakazi hao ni jambo linalostahili kusherehekewa kutokana na uhusiano wa kina baina ya Tanzania na Marekani.

"Ninaishukuru Serikali ya Tanzania na jamii washirika kwa kuipokea Peace Corps. Ni heshima kubwa kwetu kufanya kazi na watu waliojitoa kwa dhati katika nchi hii nzuri. Toka mwezi Machi 2020, wafanyakazi wa Peace Corps duniani kote wamekuwa wakifanya kazi ya kuimarisha misingi ya taasisi yetu.

"Sasa tupo tayari kuzindua tena huduma ya wafanyakazi wa kujitolea na kuadhimisha wakati huu wa kihistoria pamoja na jamii washirika wetu na wafanyakazi wetu wa Peace Corps," alisema Stephanie.

Taarifa hiyo ya Ubalozi ilibainisha kuwa baada ya mafunzo ya wiki 11 yatakayojumuisha mafunzo ya lugha ya Kiswahili, utamaduni wa Kitanzania na ujuzi mahsusi wa kiufundi kulingana na sekta zao, wataapishwa kuwa wafanyakazi wa kujitolea ili kuanza miezi yao 24 ya utoaji huduma.

# Serikali kuufuta usajili shule zilizofanya udanganyifu mtihani

**Na Waandishi Wetu,** MWANZA

SERIKALI imeagiza kufanyika uchunguzi wa kina kuhusu shule nne zilizofanya udanganyifu kwenye mtihani wa kidato cha nne mwaka wa masomo 2022, ikiwamo Shule ya Sekondari Thaqafa iliyoko jijini Mwanza na kufutiwa usajili wake kutokana na udanganyifu uliosababisha zaidi ya wanafunzi 300 kufutiwa matokeo ya mtihani huo.

Vilevile, imeagiza maofisa wote waliohusika kwenye udanganyifu huo wachukuliwe hatua kali ikiwamo kufukuzwa kazi.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda aliagiza hayo jijini Mwanza jana alipokutana na wazazi wa wanafunzi 140 walifutiwa matokeo ya mitihani yao kwa kile kinachoelezwa walifanya udanganyifu kwenye mtihani huo.

Prof. Mkenda alisema uchunguzi wa awali umebaini kuwa baadhi ya walimu kwenye shule hizo walihusika kwa asilimia 100 kufanya udanganyifu huo kwa kuwafundisha majibu wanafunzi ili wakajaze kwenye mtihani huo wa taifa.

"Ushahidi tulionao kwa sasa sio wa mfanano wa majibu pekee, vilevile tunao ushahidi wa mwalimu ambaye alikuwa akiwafundisha majibu wanafunzi hao na wanafunzi wenyewe wamemtaja, hivyo hiyo inadhihirisha uhusika wa shule licha ya shule kuchukua hatua za kumfukuza mwalimu huyo ambaye tayari ametiwa mbaroni," alisema.

Prof. Mkenda alisema baada ya kutoa agizo hilo kwa Kamishna wa Elimu nchini, aliwataka wazazi wa wanafunzi katika shule hizo kuwaondoa mapema iwezekanavyo kabla ya shule hizo kufutiwa usajili wake, ili wanafunzi hao waendelee kupata elimu bila bughudha.

Alitaja shule nyingine ni za Sekondari Twiboke ya mkoani Mara na Memoric Academy Zanzibar.

Ufafanuzi wa serikali umekuja siku chache baada ya wazazi wa wanafunzi wa 140 wa Shule ya Sekondari Thaqafa jijini Mwanza kuandamana kwenye shule hiyo kujua hatima ya watoto wao huku wakihitaji kukutana na waziri mwenye dhamana awasaidie kutatua tatizo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, aliwataka wazazi kuzungumza na watoto wao kuhusu ukosefu wa maadili pindi wanapokuwa shuleni, ikiwa ni sehemu ya njia ya kudhibiti vitendo vya wizi wa mitihani sambamba na kupambana na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia.

Jumla ya wanafunzi 162 wa shule ya Sekondari Thaqafa walifanya mtihani wa kumaliza kidato cha nne mwaka 2022. Kati yao, 22 matokeo yao yalitoka na 140 walifutiwa matokeo yao kwa kile kilichoelezwa walifanya udanganyifu kwenye mtihani huo uliofanyika Oktoba mwaka jana.

***Imeandaliwa na Neema Emmanuel na Vitus Audax**

## HABARI KITAIFA

# Xi atuma ujumbe wa pongezi kwa Mkutano wa 36 wa AU

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Xi Jinping wa China Jumamosi alituma ujumbe wa pongezi kwa Mkutano wa 36 wa Umoja wa Afrika (AU).

Katika ujumbe wake, Rais Xi alidokeza kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, AU imeungana na kuziongoza nchi za Afrika kutatua kikamilifu changamoto za kimataifa, kuharakisha ujenzi wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA) na kuwa na nafasi muhimu katika upatanishi wa masuala ya mizozo.

Aliongeza kuwa hadhi ya kimataifa na ushawishi wa Afrika umeendelea kuongezeka.



"Ninazitakia kwa dhati nchi za Afrika na watu mafanikio makubwa katika kuelekea kwenye maendeleo na ufufuaji," alisema Xi.

Rais wa China amesisitiza kuwa uhusiano kati ya China na Afrika umedumisha kasi nzuri ya maendeleo mwaka 2022 kwani ushirikiano kati ya China na Afrika umeendelea kustawi kwa pande zote, ngazi mbalimbali na ubora wa hali ya juu na iko mstari wa mbele katika ushirikiano wa kimataifa na Afrika.

Xi amesema yuko tayari kufanya kazi na viongozi wa Afrika ili kuimarisha zaidi urafiki na ushirikiano kati ya China na Afrika, kuratibu na kushirikiana kwa karibu katika masuala ya kimataifa na kikanda na kuhimiza ujenzi wa jumuiya ya ngazi ya juu ya China na Afrika yenye mustakabali wa pamoja. **(Chanzo: CGTN)**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SHINYANGA**
**MAOMBI MADOGO NA.112 YA MWAKA 2022.**

**1. DORNALD JEREMIAH IGULU................WALETA MAOMBI.**
**2. JOSEPHAT MNIKO MARWA.**

**DHIDI YA**

**PAN AFRICAN MINING SERVICES LTD................MJIMBU MAOMBI.**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**PAN AFRICAN MINING SEVICES LTD**
**POPOTE ULIPOO**

Unafahamishwa kwamba, waleta maombi tajwa hapo juu wamefungua maombi ya kukaza hukumu dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Shinyanga.

Maombi hayo yamepangwa kutajwa tarehe 06/03/2023 saa 2:30 asubuhi katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili siku hiyo wewe mwenyewe, Wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu maombi hayo.

FAHAMU KWAMBA, kushindwa kufika, Baraza litasikiliza maombi hayo na kutoa uamuzi bila ya wewe kuwepo.

IMETOLEWA kwa AMRI na CHAPA ya Baraza hili leo tarehe 06 Februari, 2023.

C. HATSON
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
SHINYANGA


# Sababu Mch. Kimaro kupewa likizo ya siku 60 zatajwa

**Na Mary Geofrey**



MCHUNGAJI wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Usharika wa Kijitonyama, Dk. Eliona Kimaro, amesamehewa adhabu yake ya likizo ya siku 60 akiwa ameitumikia kwa siku 34 hadi jana.

Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, alitangaza msamaha huo jana.

Mch. Kimaro alikutana na msamaha huo aliposhiriki ibada ya shukrani katika Usharika wa Kinyerezi, Tabata jijini Dar es Salaam iliyoongozwa na Askofu Malasusa.

Kusimamishwa kwa Mch. Kimaro kulianza kufahamika usiku wa Januari 16 mwaka huu kupitia video iliyokuwa inasambaa ikimwonyesha akiwaaga waumini wa ibada ya masifu ya jioni, kuwa amepewa likizo ya siku 60 baada ya kuitwa kwenye ofisi ya msaidizi wa askofu na kufanya kikao na mkuu wa jimbo.

Katika video hiyo, Mch. Kimaro alitangaza kumaliza likizo yake Machi 17 mwaka huu na baada ya likizo, atatakiwa kuripoti Makao Makuu ya Dayosisi na sio kwenye usharika huo tena, huku akiacha sintofahamu kwa waumini bila kufahamu sababu.

Katika msamaha uliotangazwa jana wakati wa ibada hiyo, Mch. Kimaro alipewa nafasi ya kusalimia waumini hao akiwa kama mchungaji mshiriki wa ibada na ndipo alitumia fursa hiyo kuomba radhi na kueleza sababu za adhabu aliyopewa.

"Nitumie fursa hii kwa moyo wa unyenyekevu na ninasikia kunyenyekea sana ndani ya moyo wangu, kuwaomba sana radhi na msamaha kwa Baba Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Alex Malasusa kwa mambo mengi yaliyoendelea na yaliyosikika kwenye mitandao ya kijamii na mengine hayakuwa na sura nzuri," alisema.

Mchungaji huyo alisema kuwa Novemba 13, mwaka jana, akiwa kwenye ibada ya mavuno katika Usharika wa Kijitonyama, aliongoza ibada na kuhubiri, kuwaombea wanafunzi wa kidato cha nne na vijana wasio na ajira.

"Mwishoni nilisukumwa kuwaombea wale vijana wasio na ajira na nilisisitiza suala la nidhamu, 'Seif Discipline' (nidhamu binafsi) na 'life Discipline' (nidhamu ya maisha) na katika kusisitiza, niliitoa mfano wa vijana wa usharika wangu wa Kijitonyama na wale wa dhehebu lingine, labda nitamke wazi wale wa Kiislamu.

"Baada ya hapo yale maneno yalinukuliwa kwa kukatwa huko duniani na watu nisiyowajua na kutengenezwa 'clip' (video fupi) ambayo ilikuwa inaonyesha ulinganifu kati ya vijana wa Kiislamu na Wakristo katika suala la uaminifu hasa kwa vijana.

"Jambo hilo limeleta mtafaruku mkubwa ndani ya jamii na sintofahamu, wapo waliopekea 'positive' (chanya) na waliopokea 'negative' (hasi)," alisema.

Mchungaji huyo alisema amepokea uamuzi wa Askofu Malasusa kama mchungaji mwenye kiapo na nadhiri ya daima za uchungaji, kutii maelekezo ya askofu.

"Katika nidhamu ya kanisa na agizo la kanisa, lazima viongozi wa kanisa walichukue na moja ya mambo ya misingi waliyochukua ni kupata mapumziko ya kutafakari na moja kwa moja nilipokea kwa unyenyekevu na kwenda kwenye nyumba za malezi ya kichungaji na ndiko nilipotokea asubuhi ya leo (jana), nikiendelea kusali, kutafakari na kufunga," alisisitiza Mch. Kimaro.

Aliomba radhi kwa Askofu Mkuu wa KKKT, Dk. Frederick Shoo kwa usumbufu aliopata wakati akiwa likizo ya siku 60.

"Ninaomba radhi kwa wakristo wote duniani, waliokwazika kwa matamshi yangu, ninaombeni sana radhi kwa hili," alisema Mch. Kimaro.

### MALASUSA AMSAMEHE

Baada ya Mch. Kimaro kumaliza kuzungumza, Askofu Malasusa alisema kuwa kwa niaba ya washarika, Mch. Kimaro amesamehewa na aendelee kutafakari na kukaa karibu na Mungu ili shetani asimwondoe kwenye mstari.

"Ninaomba nikushike mkono, pole sana, sana, sana, sana, sana mama, ninajua pia umeumia sana (mke wa Mch. Kimaro), endeleeni kutafakari na kukaa chini ya miguu ya Mungu.

"Tunaiona huduma yenu na Mungu awatie nguvu, nitaendelea kuwaombea kwa sababu ni jukumu langu, nanyi bado ni watoto. Mungu awabariki sana, Mungu awatie nguvu," alisema Askofu Malasusa huku akiwashika mikono.

Wakati hayo yakiendelea, kanisa lililipuka kwa shangwe na vilio vya furaha kwa kile walichodai ni unyenyekevu alioonyesha Mch. Kimaro na ukomavu wa Askofu Malasusa kumsamehe.

### BANGO MOROCCO

Saa chache kabla ya msamaha huo, baadhi ya waumini walioonyesha kuumizwa na adhabu ya Mch. Kimaro, walichanga fedha kwenye kundi songezi la WhatsApp lenye jina la 'Bring Back Our Kimaro (Mrudishe Kimaro Wetu), walibandika picha yake eneo la Morocco, Kinondoni.

Bango lenye picha yake lenye maandishi yanayosomeka 'But The Greatest Of This Love' 1 Cor 13: 13 na kichwa cha habari kikubwa kinachosema 'Let There Be Light' ikiwa na maana 'Na iwe nuru', na ujumbe unaosema, 'washarika na waumini wa Kijitonyama tunakupenda'.

Bango hilo lilibandika juzi jioni na watu mbalimbali walikuwa wakipita kulipiga picha na kurusha kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
18.02.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Alhamisi tarehe 23-02-2023 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Ruvuma kupitia Mingoyo,** gari hiyo ina namba za usajili: **T 903 DSD / T 380 DHQ**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 18.00** |
| **Upana** | - | **mita 5.55** |
| **Kimo** | - | **mita 4.80** |

2. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Ruvuma kupitia Nangurukuru, Lindi, Masasi, Songea mpaka Ruvuma** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**



HAPPY Valentine's Day

**INFINIX MOBILE TZ YAACHA ALAMA KUBWA KWA MASHABIKI SIKU YA VALENTINE.**

Kampuni ya simu janja ya Infinix mobile Tz imesherehekea Siku ya Wapendanao kwa namna ya kipekee kwa kuwapa wateja wake fursa nzuri ya kuboresha mapenzi yao na wapenzi wao, kufurahia pamoja na wengine na chapa na kupata zawadi kwa ajili yao na wapendwa wao. Tukio hili limefanyika katika ukumbi maarufu wa nyota tano wa Golden Tulip Oyster Bay, ambapo wapenzi wamepata fursa ya kucheza pamoja michezo mbalimbali ya kufurahisha na wapenzi wao. Wakati wa ufunguzi wa hafla hiyo, meneja uhusiano wa umma Bw: Erick Mkomoye aliwaambia wageni maono na shabaha ya chapa (kampuni) juu ya soko la sasa 'kampuni hiyo inalenga vijana kwa asilimia kubwa' hiyo ndiyo sababu kuu ya kuendelea kuwa vijana na kusherehekea pamoja Siku hii ya Wapendanao

*Kaa na Infinix siku zijazo ni Sasa.*



117288202

# Kazi nyumbani kwa mwalimu zilivyo kichaka cha ukatili kwa wanafunzi

**Na Beatrice Shayo,** aliyekuwa KALIUA



KUNA shida gani shuleni siku hizi? Ilizoeleka shuleni ndiko mahali salama kwa watoto, hali ambayo iliwafanya wazazi na walezi wengi kuwa na imani kubwa na yanayotendeka huko.

Sasa hali inazidi kuwa tofauti kutokana na matukio mengi ya ukatili dhidi ya watoto kuripotiwa kutoka mahali huko.

Mnamo mwaka 2020, Nipashe iliripoti baadhi ya wanafunzi wilayani Mkuranga mkoani Pwani kulawitiana wakiwa shuleni na mwezi uliopita, gazeti hili limeripoti hatari nyingine ya baadhi ya shule binafsi mkoani Kilimanjaro kuwafundisha watoto kutendana 'uchafu' huo.

Si hayo, yapo matukio mengine ya ukatili dhidi ya wanafunzi, yakijumuisha vipigo vya kikatili kutoka kwa walimu wao na hata baadhi ya wanafunzi kulawitiwa na madereva wanaoendesha magari ya shule.

Unaposaka jibu la swali 'kumetokea nini shuleni siku hizi?' kutana na mkasa wa mwanafunzi aliyepewa ujauzito na mwalimu wake wilayani Kaliua mkoani Tabora miaka mitatu iliyopita.

Mtoto huyo mwenye umri wa miaka 14 (jina tunalihifadhi), anasimulia kuwa alikumbana na ukatili huo mwaka 2020 akiwa mwanafunzi wa darasa la sita kwenye Shule ya Msingi Kazana Upate iliyoko Kata ya Igagala wilayani Kaliua.

Binti huyo anasimulia kuwa siku ya tukio, mwaka 2020, majira ya saa saba mchana, mwalimu huyo (jina tunalo) alimtaka aende kuosha vyombo nyumbani kwake na alipotaka kuongezwa wanafunzi wenzake wa kumsaidia kufanya kazi hiyo, mrejesho kutoka kwa mwalimu ulikuwa "utawakuta huko nyumbani".

Anasema kuwa baada ya kufika kwenye makazi hayo ya mwalimu ambayo hayakuwa mbali na shule, mwalimu huyo alitoka shuleni na kumfuata ndipo alipomwuliza 'mbona wenzangu (wanafunzi) siwaoni?'

"Nilimuuliza wanafunzi wenzangu wako wapi ili nikaoshe nao vyombo, akaniambia wapo humo ndani, fungua mlango utawakuta waambie watoe vyombo mwoshe. Nilipoingia ndani, sikuwakuta wanafunzi wenzangu, akabana mlango.

"Baada ya kufunga mlango, aliniziba mdomo maana nilikuwa ninapiga kelele, akanipeleka chumbani na kuanza kunibaka, sikuwa ninaelewa chochote, nilijikuta ninapata maumivu makali, baada ya hapo akanipa buku jero (Sh. 1,500) nikanunue dawa za maumivu.

"Nilikuwa sijawahi kwenda kuosha vyombo kwa mwalimu huyo kwa kuwa ana mke ambaye ni dada yangu, mtoto wa mama mkubwa.

"Mwalimu nilimwacha shuleni, sasa sijui alichukua baiskeli ya kuniwahi nyumbani maana alijua kabisa wenzangu hawapo, lakini akaniambia nitawakuta wakati hawapo nyumbani kwake.

"Ninafikiri aliamua kunidanganya kwa staili hiyo maana wanafunzi huwa tukienda kuosha vyombo kwa walimu, tunakuwa wengi, siyo mwanafunzi mmoja, ndiyo maana nilimwuliza kuhusu wenzangu," anasimulia.

Anadai kuwa baada ya kupewa Sh. 1,500, mwalimu huyo alimtishia asiseme kwa wazazi wake na akifanya hivyo, atampatia adhabu kila siku na kumwachisha shule, hivyo aliogopa kuwajulisha alichofanyiwa huku akiwa anaugulia maumivu.

"Hiyo siku ilikuwa ndiyo mara yangu ya kwanza, nilipatwa na maumivu makali na alinitishia nisiseme kwa wazazi wangu. Nilipotoka pale nikarudi shuleni kuendelea na masomo, ulipofika muda wa kurudi nyumbani, nilirejea nyumbani nikaogopa.

"Ninakumbuka tulitoka shuleni majira ya saa 10:30 jioni, niliogopa kuwasimulia wazazi wangu kutokana na vitisho nilivyopatiwa na mwalimu," anasema na kubainisha kuwa mwalimu huyo alikuwa anafundisha masomo ya Hisabati na Maarifa ya Jamii.

Binti huyo anarejea uhusiano wake kimasomo na mwalimu huyo, akisema kuwa awali alikuwa anamchangamkia, lakini baada ya kufanya kitendo hicho, 'walikata mawasiliano na uchangamfu'.

Anafafanua namna wanafunzi wanavyofanya kazi za nyumbani kwenye makazi ya walimu, akitamka: "Ratiba yetu ya shuleni inaanzia asubuhi, saa 6:30 mchana mpaka saa 7:45 mchana hakuna masomo, hivyo tunarudi nyumbani kwa ajili ya kula chakula cha mchana.

"Huu muda sio wa masomo ila inavyofika muda wa mapumziko saa 9:20 alasiri, kengele hugongwa kwa ajili ya mapumziko, wakati huo ndipo walimu huchagua darasa fulani kwa ajili ya kuchota maji ya walimu na kuosha vyombo vyao," anasema.

### UPATA UJAUZITO

Mficha maradhi, kifo humwumbua! Binti huyo aliyelazimika kuficha ukatili aliotendwa na mwalimu wake, anasema hakufahamu chochote zaidi ya kujishangaa maziwa yake kujaa, akijua yupo kwenye hatua ya ukuaji.

"Sikugundua kama nina ujauzito ila nilikuwa ninapata usingizi kila mara, ninashindwa kufanya kazi nyumbani, muda wote ninakuwa mvivu, ni kulala tu, maziwa yalikuwa yanajaa, nikajua ninakua 'mdada'.

"Kutokana na mabadiliko hayo, mama alinishtukia na kunipeleka kituo cha afya kwa ajili ya kufanyiwa vipimo, nikagundulika nina ujauzito wa miezi mitatu, sikumbuki tarehe niliyofanyiwa vipimo kwa sababu muda umepita," anasema binti huyo aliyehojiwa na Nipashe wilayani Kaliua mwishoni mwa mwaka jana.

Anasema majibu ya vipimo hivyo yakafuta ndoto zake kimasomo, akakatisha masomo yake na sasa yuko nyumbani analea mtoto wake wa kiume mwenye umri wa miaka miwili.

Takwimu za Ofisi ya Rais -TAMISEMI za mwaka 2020, zinaonyesha kuwa mwaka 2015 hadi 2019, wanafunzi wa kike 28,914 nchini walikatisha masomo kutokana na sababu ya ujauzito. Kati yao, wa shule ya msingi walikuwa 4,205 na wa sekondari walikuwa 24,709.

### BABA ANENA

Baba mlezi wa binti hiyo, Emmanuel Mhembano (57) anasema amekuwa anaishi naye tangu binti huyo akiwa na umri wa miaka mitatu.

"Mama yake huyu mtoto alichana na baba yake ndipo nikamwoa. Wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 tulijua binti yetu ana ujauzito, baada ya kumbana akamtaja mwalimu huyo.

"Tulibaini binti yetu ana mabadiliko na tulipomhoji baada ya kujiridhisha kwa vipimo vya zahanati, hakuwa tayari kueleza kutokana na vitisho alivyopewa na mwalimu huyo.

"Tumpeleka Zahanati ya Igagala na kufanyiwa vipimo na kujulikana ana ujauzito wa miezi mitatu, tulipombana kwa kina, akamtaja mwalimu wake ambaye alidai alimtishia asiseme alichomfanyia.

"Baada ya kupata taarifa hizo, nilizijulisha ngazi ya serikali na vyombo vya dola Oktoba 31, mwaka 2020, ili hatua zichukuliwe.

"Mwalimu huyo alikamatwa na kesi kufunguliwa Mahakama ya Wilaya na baadaye ilihamishiwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Tabora," anasimulia.

### WATENDAJI SERIKALINI

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kazana Upate, Thabiti Kasagula, anakiri kuwa na taarifa za tukio hilo kijijini kwake.

"Askari polisi walitumwa wakamkamata mwalimu na kupelekwa Kituo cha Polisi Igagala na baadaye alihamishiwa kituo kikubwa cha Kaliua na kesi kupelekwa mahakama ya wilaya ilikotolewa ushahidi," anasema na kubainisha kuwa mwalimu huyo alisimamishwa kazi wakati kesi hiyo inaendelea kortini.

Ofisa Tarafa wa Igagala, Saimon Marando, pia anakiri kuwa na taarifa za tukio hilo, akieleza kuwa alikuwa sehemu ya walioshiriki kukamilisha mchakato wa kufungua kesi kortini.

Marando anasema alimwomba mlezi wa mtoto huyo kuhakikisha kesi inavyokwenda mahakamani, atoe ushirikiano katika ushahidi.

### KESI JUU YA KESI

Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Paul Chacha, baada ya kupata taarifa za tukio hilo, aliagiza kesi kuanza upya mahakamani, akidai kuna mashtaka zaidi.

Alidai kuwa mbali na kudaiwa kukatisha masomo ya mwanafunzi huyo wa darasa la sita kwa kumpa ujauzito, mwalimu huyo pia anadaiwa kukatisha masomo ya mwanafunzi wa kidato cha pili na kumwoa ambaye ni ndugu wa mwanafunzi aliyepewa ujauzito.

"Mungu amemuumbua, akamrubuni huyu mwanafunzi. Walimu huwa wanawatuma watoto 'nenda kanifanyie kazi nyumbani', akamwambia aende kumwoshea vyombo nyumbani. Alimfuata na kumbaka na hiyo siku ndipo alipopata ujauzito.

"Baba mlezi wa mtoto huyo alipambana kwenda kutafuta haki na kesi ilifika mahakamani ya wilaya, baadaye kesi hiyo ikachezeshwa.

"Hii kesi baadaye sijui ikawaje, mara sijui faili halionekani, ni namna ya kuficha, yaani mara kesi imetoka mahakamani nilivyokuja nikiwa ni mgeni nikajaribu kufuatilia, nikamwita huyo mzee, alikuja kwa bahati mbaya hakunipata nikatoa maelekezo hata kama nitakuwa nimekosea, niliagiza huyu mwalimu akamatwe," alidai Chacha.

Mkuu wa Wilaya anasema ameshaelekeza mtoto huyo arudishwe shuleni na kwamba kuna taratibu ambazo zinaendelea na Ofisa Elimu wameshakubaliana analifanyia kazi suala hilo.

"Pia nimesema nitamsimamia mimi kwa chochote ambacho kitakuwa kinahitajika, kama malipo yoyote, sare za shule, sijui madaftari, nitavifanya hata kama nitatoka katika hii wilaya, nitamkabidhi kwa DC (Mkuu wa Wilaya) kuhakikisha ndoto yake ya kusoma inaendelea," anasema.

### WALIOOA WANAFUNZI

Chacha pia anabainisha kuwa mwaka jana wanafunzi 3,700 waliofaulu kujiunga na shule za sekondari wilayani Kaliua, hawakuripoti shuleni na walipofuatilia, walibaini wanafunzi 800 walikuwa wameolewa na tayari takriban nusu ya waliowaoa wanafunzi hao, wamefikishwa kwenye vyombo vya dola.

"Asilimia 50 ya waliowaoa wanafunzi hao wamefikishwa kwenye vyombo vya dola, hawa wengine tuliwakuta wapo Bariadi, Simiyu tukawarudisha, mazingira ni haya tunayopambana nayo. Kuna shida ila jamii hii ina mtazamo hasi kuhusu elimu. Wakimwona binti amekua, hawa wafugaji wanaona binti ni wa kuolewa badala ya kwenda shuleni," anasema Chacha.

### SAUTI ZA WADAU

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, anampongeza Mkuu wa Wilaya Chacha kwa hatua anazochukua kuhakikisha haki za mabinti zinalindwa.

Anna ambaye ni mwanasheria kitaaluma, anasema suala la walimu kuwafanyisha kazi wanafunzi haliruhusiwi kisheria na jambo hilo limekuwa tatizo kwa walimu wengi, hasa maeneo ya vijijini.

Anasema kuwa wengi wanawafanyisha kazi wanafunzi na matokeo yake wanakutana na vitendo viovu kama kilichomkuta mwanafunzi huyo wa Kaliua.

# TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED

**'We light Up Your Life'**

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST (REOI)**
**FOR**
**TENDER NO. PA/001/2022-23/HQ/C/34**
**BORROWER'S REF. NO.: TZ-TANESCO-323445-CS-INDV**
**FOR**

## PROVISION OF CONSULTANCY SERVICES TO PROVIDE SUPPORT AS CONTRACT MANAGER FOR THE IMPLEMENTATION OF CORPORATE MANAGEMENT SYSTEM (CMS) UNDER TANZANIA – ZAMBIA TRANSMISSION INTERCONNECTOR PROJECT (TAZA) – INDIVIDUAL CONSULTANT

**FEBRUARY, 2023**

**Plot 114, Block G, Dar es Salaam Road**
**P.O. Box 453, Dodoma, Tanzania.**
**Email: md.tanesco@tanesco.co.tz**
**Cc: pmuhq@tanesco.co.tz**

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST (REOI) FOR ENGAGEMENT OF CONTRACT MANAGER UNDER THE TANZANIA – ZAMBIA TRANSMISSION INTERCONNECTOR PROJECT (TAZA)**

**Project Name: TANZANIA – ZAMBIA TRANSMISSION INTERCONNECTOR PROJECT (TAZA)**

**Assignment Title: Provision of Consultancy Services to Provide Support as Contract Manager for the Implementation of Corporate Management System (CMS) under Tanzania – Zambia Transmission Interconnector Project (TAZA) - Individual Consulting Service**

**Tender No.: PA/001/2022-23/HQ/C/34**

**BORROWER'S REF. NO.: TZ-TANESCO-323445-CS-INDV**

**Issue Date: 17/02/2023**

1. The Government of the United Republic of Tanzania through Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO) has received financing from the World Bank toward the cost for provision of consultancy services to support contract's management activities for Implementation of Corporate Management System (CMS) under the Tanzania – Zambia Transmission Interconnector Project (TAZA).

2. The consulting services ("the Services") include but not limited to supporting the Client, particularly the Project Manager and relevant professional staff for the Tanzania - Zambia Transmission Interconnector Project (TAZA) in planning, preparations, and management of Corporate Management System (CMS) and other contracts indicated in the TOR. The individual consultant shall also be responsible for supporting the Client on ensuring that all activities are implemented and managed in accordance with the terms, conditions and other requirements indicated in the respective contracts.

3. The detailed Terms of Reference (TOR) for this assignment are available on the following websites: https://www.taneps.go.tz and TANESCO Website https://www.tanesco.co.tz. The Consultants are required to register on TANePS in order to be able to participate in this selection process. All requests for clarification shall be sent through TANePS and the Client will send Responses to Clarifications and Amendments through TANePS - https://www.taneps.go.tz, TANESCO Website https://www.tanesco.co.tz and email notification will also automatically be sent to those Consultants who have started working on this Request for Expression of Interest through TANePS. The Consultants shall be responsible for ensuring that any addenda available on the website is also downloaded and incorporated.

4. TANESCO now invites eligible Individual Consultants to indicate their interest in providing the Services. Interested Individual Consultants shall provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the Services. The shortlisting criteria are: -

   (a) A Minimum Bachelor's Degree in Engineering, Procurement, Business Administration, Commerce, Economics, Finance, or any other related field from a recognized institution coupled with extensive and demonstrated experience managing power transmission infrastructure works contracts of 132kV voltage level and above.
   (b) A strong experience of at least ten (10) years' work experience managing large contracts for power transmission infrastructure works at 132kv and above;
   (c) Knowledge of the relevant FIDIC guidelines will be an added advantage;
   (d) Good oral, written and fluent communication skills in English Language;
   (e) A high level of interpersonal and management skills and ability to work independently, unsupervised and also with teams in the organization at all levels;
   (f) Must be able to work under pressure with tight deadlines;
   (g) Computer knowledge and skills in MS Word, MS Excel, is a mandatory requirement;
   (h) Excellent in Project Management Using Microsoft Project Professional 2019 Software at minimum;
   (i) Proven integrity and confidentiality in handling public resources and in executing duties; and
   (j) The candidate should be Eligible and have no Conflict of Interest (CoI) as per World Bank's Procurement Regulations for IPF Borrowers, Fourth Edition, November 2020, Section III – Governance; Sub-section 3.21 for eligibility and Sub-section 3.14 to 3.16 for Conflict of Interest.

5. The attention of interested Individual Consultants is drawn to Section III, paragraphs, 3.14, 3.16, and 3.17 of the World Bank's "Procurement Regulations for IPF Borrowers" November, 2020 – Fourth Edition setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.

6. Individual Consultant will be selected in accordance with the procedures set forth in the Procurement Regulations.

7. Interested individual consultants must also provide information indicating that they are qualified to perform the services by submitting ***individual consultant's profile, description of similar assignments, experience in similar conditions and evidence of appropriate skills.***

8. Expressions of Interest must be submitted online through Tanzania National Electronic Procurement System (TANePS) (www.taneps.go.tz) on or before **Friday, 17th March, 2023 at 14:30 Hours, East African Time.** Please, remember to attach all necessary supporting documents including but not limited to Academic and Training Certificates. The Client shall not be held liable for any delays due to system failure beyond its control. Even though, the system will attempt to notify the Consultants of any updates, the Client shall not be liable for any information not received by the bidder. It is the Consultants' responsibility to verify the website for the latest information related to this selection process. Expression of Interests will be opened promptly thereafter through **TANePS.**

The Application Letter which shall be submitted on TANePS must be addressed to:

**Secretary Tender Board**
**Tanzania Electric Supply Company Limited**
**Umeme Park Building, Third Floor, Room No. 310**
**Morogoro Road, Ubungo Area,**
**Dar es Salaam, TANZANIA**
**Attn: Ms. Rehema O. Shabani**
**P. O. Box 9024**
**Dar es Salaam, TANZANIA**
**Tel: +255 22 221 0231, +255 22 221 0232**
**E-mail: sec.tenderboard@tanesco.co.tz ; pmuprojects@tanesco.co.tz**
**Web Site: www.tanesco.co.tz**

217287501

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uwekezaji mkubwa unahitajika Simba, Yanga michuano CAF

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), Simba na Yanga wameanza vibaya katika kinyang'anyiro cha Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho baada ya zote kupoteza ugenini kwenye mechi za awali za hatua ya makundi.

Simba ambayo inaiwakilisha Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, ilianza kwa kukubali kipigo cha bao 1-0 ugenini dhidi ya Horoya AC ya Guinea kabla ya kurejea nyumbani na juzi kuchapwa mabao 3-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco.

Matokeo hayo yanaifanya Simba sasa kubakiza michezo miwili nyumbani dhidi ya Horoya AC na Vipers ya Uganda huku ikiwa na mechi mbili pia ugenini dhidi ya Waganda hao na Raja Casablanca.

Watani zao, Yanga ambao wanaiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, wenyewe jana usiku walitarajia kuikaribisha TP Mazembe ya DR Congo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa ikiwa ni baada ya kuchapwa mabao 2-0 ugenini dhidi ya US Monastir ya Tunisia katika mchezo wa awali.

Baada ya mechi ya jana usiku, Yanga nayo inabakiza michezo miwili nyumbani dhidi ya US Monastir na Real Bamako ya Mali, wakati pia ikiwa na mingine idadi kama hiyo ugenini dhidi ya miamba hiyo ya Mali na TP Mazembe.

Kwa ujumla kwa viwango vilivyoonyeshwa na wawakilishi hao wa nchi, bila kujali matokeo ya mechi ya jana usiku kati ya Yanga na TP Mazembe, inaonyesha bado kunahitajika uwekezaji mkubwa husasan kwa upande wa usajili wa wachezaji wenye viwango vikubwa zaidi wanaoweza kuzipa matokeo chanya katika michuano hiyo.

Wachezaji wengi wanaosajili na timu zetu hususan Simba na Yanga, ni wale ambao tayari wameshindwa kufanya vizuri katika klabu kubwa za nje ambazo ndizo wanapambana nazo kwenye michuano hiyo ya CAF, jambo ambalo linazifanya kupata wakati ugumu wa kushinda kutokana na kuzidiwa ubora.

Tunatambua ni vigumu kwa klabu za Tanzania kuweza kuonyesha msuli katika vita vya kuwania kusajili wachezaji wazuri dhidi ya klabu kubwa za Kaskazini (Uarabuni), ambazo zina nguvu kubwa kiuchumi, lakini Nipashe tunaona bado inawezekana kupata wachezaji wazuri wanaoweza kutoa ushindani dhidi ya miamba hiyo kama zitawekeza katika wataalamu.

Tunaamini kinachozifelisha klabu zetu ni kukosa wataalamu wazuri katika idara zao za usajili, ambao wanatumia msimu mzima kufuatilia baadhi ya nyota wanaowahitaji kusajiliwa pindi dirisha la usajili linapofunguliwa.

Pamoja na timu za Kiarabu kuwa na nguvu kubwa kiuchumi, bado haziwezi kusajili wachezaji wote bora barani Afrika, hivyo kinachotakiwa kwa klabu zetu ni kuwekeza wataalamu zaidi katika idara zao za usajili ili na hapo zinaweza kupata wachezaji wenye vipaji ambao si tu watazisaidia kwenye michuano ya kimataifa kama hiyo, bali wataziingizia fedha nyingi kwa kuwauza hapo baadaye.

Mara nyingi, klabu za Tanzania husasan Simba na Yanga, hutegemea kumuona mchezaji katika mechi moja ama mbili tu alizoichezea klabu yake tena ilipocheza na moja kati ya hizo mbili na kuifunga, jambo ambalo si kipimo sahihi cha kutosha kumsajili mchezaji.

Hivyo, bila Simba, Yanga na klabu zingine za Tanzania kubadili mfumo wao mzima wa usajili, zitaendelea kuumia kila msimu kwa kushindwa kufika mbali kwenye michuano hiyo ya kimataifa yenye utajiri mkubwa na inayovutia mashabiki wengi kwenda uwanjani kuzishangilia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba isikate tamaa, nafasi CAF bado ipo kama ikiamua

Na Adam Fungamwango

**BAADHI** ya wanachama na mashabiki wa Simba wameonekana kukata tamaa kwa timu yao kusonga mbele kwenye hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika, baada ya kufungwa mabao 3-0 na Raja Casablanca kutoka nchini Morocco juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mashabiki wa timu hiyo walijazana kwenye uwanja huo, ambapo walikuwa wakibebwa na kaulimbiu ya 'Kwa Mkapa Hatoki Mtu.'

Ni kweli, Simba imekuwa ikiutumia vema uwanja huo kwenye michezo mbalimbali ya kimataifa, hasa mechi ngumu, lakini imekuwa ikifungwa mara chache.

Kwenye mechi dhidi ya Raja Casablanca ilionekana ni mfupa mgumu kwa Simba, si kwa sababu wachezaji wao hawakucheza vema, lakini kiwango kikubwa kilichoonyeshwa na wageni, kilionyesha utofauti kati ya viwango vya wachezaji wa timu hizo mbili.

Hii ni ishara kuwa ili timu za Tanzania zifanye vema kwenye michuano hiyo ni lazima timu iwe na wachezaji wa viwango vinavyotakiwa. Zinatakiwa zipate wachezaji wenye kusaka matokeo ambao ni hatari na si machachari.

Hapa inaonyesha kuwa gharama zinatakiwa kupata baadhi ya wachezaji wenye viwango vikubwa zaidi ya hao waliokuwapo.

Baada ya mechi hiyo, Simba inakamata nafasi ya mwisho kwenye msimamo Kundi C ambalo lina timu hizo, pamoja na Horoya AC ya Guinea na Vipers ya Uganda.

Wakati Raja Casablanca ikiwa na pointi sita, Horoya ina nne, Vipers baada ya suluhu nyumbani ina pointi moja, huku wawakilishi wa hao wa Tanzania wakiwa hawana pointi yoyote.

Kwa jinsi nilivyoiona Raja Casablanca, kama ikiamua, inaweza kushinda mechi zote sita za kundi hilo, yaani kuzifunga timu zote tatu nyumbani na ugenini. Ni timu iliyo kwenye kundi ambalo lina timu ambazo hazipo kwenye viwango vyake.

Kwa maana hiyo basi kwenye kundi hili wala haina shaka kuwa 'Waarabu' hao wameshaichukua nafasi ya kwanza na sasa timu tatu za Simba, Horoya na Vipers ndiyo wanaisaka nafasi moja iliyobaki.

Wala siidai Simba kwa lolote lile kwa kupoteza mechi dhidi ya Raja Casablanca juzi, lakini nawalaumu kwa kushindwa kushinda au kupata sare nchini Guinea ilipocheza dhidi ya Horoya kwa sababu mechi ile ilikuwa mikononi mwao.

Nadhani sasa itajifunza kitu kimoja kuwa isitegemee sana kushinda nyumbani, kama kuna uwezekano wa kupata pointi tatu ugenini zoa tu.

Wakati wengi wakiikatia tamaa Simba, binafsi naona bado timu hiyo ina nafasi na kutinga hatua ya robo fainali kama inazichanga karata zake vizuri kwenye mechi tatu mfululizo itakazokwenda kucheza.

Februari 25 itakwenda nchini Uganda kucheza dhidi ya Vipers na Machi 7, itacheza tena dhidi ya timu hiyo hiyo Uwanja wa Benjamin Mkapa, kabla ya kukutana na Horoya Machi 17 hapa hapa nchini.

Hizi ndizo mechi za Simba kucheza karata yake vizuri kwani timu inazocheza nazo ziko chini ya uwezo wao kama viongozi watafanya maandalizi mazuri na wachezaji wakacheza kwa kujituma na kuusaka ushindi kwa udi na uvumba.

Waitoe kabisa mechi ya mwisho dhidi ya Raja Casablanca nchini Morocco, ambayo sidhani kama Simba inaweza kwenda kupata hata pointi moja, ingawa kwenye soka lolote linaweza kutokea.

Simba inatakiwa kupata pointi sita dhidi ya Vipers ambapo hilo kwao linawezekana, halafu pia ina uwezo wa kupata ushindi dhidi ya Horoya na kukusanya pointi tisa.

Hapo mpinzani wake mkubwa atakuwa Horoya, ambayo sidhani kama inaweza kwenda kushinda Morocco, hivyo itabaki na pointi nne. Itarudiana tena na Raja Casablanca ambapo kwa asilimia kubwa mgeni anaweza kushinda au sare, hivyo kuwa na pointi tano.

Horoya ina uwezo wa kuifunga Vipers nchini Guinea, hivyo inaweza kufikisha pointi nane. Ikifungwa dhidi ya Simba, inamaliza ikiwa na pointi hizo na Simba itakuwa na tisa. Hayo ni mahesabu ya vidole ambayo yanaweza kuifanya Simba kutinga robo fainali na kwa viwango vya timu husika, matokeo niliyoyataja inawezekana kabisa.

Kikubwa ni Simba kujifunga kibwebwe kwa mechi tatu zilizobaki. Kufungwa au sare yoyote ni dhahiri kuwa itakuwa haina chake msimu huu kwenye michuano hiyo ambayo mara kwa mara imekuwa ikifika robo fainali.

# Mbunge atua mzigo wazazi michango mitihani shuleni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, ametoa vifaa na fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo mashine za kuchapisha mitihani ili kuwaondolea mzigo wazazi waliokuwa wakilazimika kuchangia kila wiki uchapishaji kwenye shule za umma.

Msaada huo umetolewa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo.

Akizungumza katika makabidhiano ya vifaa hivyo jana, Mavunde ambaye ni Naibu Waziri wa Kilimo, alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23, jimbo hilo limepokea Sh. milioni 93.8 ambazo zimeelekezwa kwenye miradi ya maendeleo na kununua mashine kwa tarafa nne za Jiji la Dodoma na kuwekwa kwenye vituo vya umahiri wa majaribio ya mitihani.

"Kila ninapopita kwenye mikutano ya hadhara wazazi wanalalamika michango licha ya kukaa vikao na kukubaliana kuchangia uchapishaji mitihani, nikaona nipunguze mzigo ili ofisi ya mbunge kupitia mfuko wa jimbo ibebe dhamana hiyo na kutatua changamoto hiyo na tutaweka utaratibu mzuri wa kila tarafa kuwa na sehemu yao ya uchapishaji mitihani na ninatoa na rimu za kuanzia 200.

"Ninaishukuru serikali imetuongezea fedha za mfuko wa jimbo, haijawahi kutokea na zimesaidia sana hasa majimbo makubwa kama la Dodoma Mjini, tumeongezewa kutoka Sh. milioni 70 hadi 93.8, tulishaweka malengo kwenye fedha hizi kipaumbele ni elimu, afya na uwezeshaji wananchi kiuchumi," alisema.

Alieleza kuwa fedha hizo mbali na kununua mashine hizo, pia zitatumika kujenga madarasa na vivuko vya wanafunzi kwenye kata ambazo zimekuwa zina tatizo hilo na kusababisha wananchi hasa wanafunzi kushindwa kuvuka kwenda shuleni.

"Ujenzi wa vivuko utafanyika Kata za Tambukareli na Dodoma Makulu ili kuhudumia wanafunzi wa Shule ya Sekondari Sechelela, ujenzi wa madarasa utafanyika Shule ya Msingi Kunambi, Mbuyuni-Kizota, Shule mpya ya Sekondari ya Matumbulu na Shule ya msingi Michese-Mkonze," alisema.

Alifafanua kuwa fedha hizo kwa mwaka 2016/17 zilitolewa kwa ajili ya vikundi vya kinamama na vijana kwa kuwezeshwa mashine za kutotolesha vifaranga, matofali, kutengeneza juisi na za kunyonyolea kuku.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Vodacom Tanzania, Philip Besiimire, akiambatana na watumishi wengine wa kampuni mkoani Mbeya kwa ajili ya kukagua, kuwatembelea na kuwasikiliza wateja na watoa huduma maeneo ya Kabwe jijini Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampeni ya CRDB kuongeza ujumuishi huduma za kifedha

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

WAKAZI wa Moshi mkoani Kilimanjaro wameonekana kuipokea vyema promosheni ya 'Benki ni SimBanking' ikiwa ni sehemu ya jitihada za Benki ya CRDB kuongeza ujumuishi wa Watanzania kwenye huduma za kibenki.

Wakazi hao walijitokeza kwa wingi katika uzinduzi wa promosheni hiyo mkoani Moshi wiki iliyopita, walionyesha kufurahia huduma zinazopatikana katika huduma ya SimBanking ambazo kwa kiasi kikubwa zimeondoa ulazima wa mteja kutembelea matawi ya benki, iwe kufungua akaunti au kufanya miamala.

Akizungumza na mamia ya wateja waliojitokeza katika uzinduzi wa promosheni hiyo, Kaimu Meneja wa Kanda ya Kaskazini wa Benki ya CRDB, Emmanuel Kafui, alisema kuwa anatamani kuona huduma ya SimBanking inakuwa sehemu ya maisha ya kila siku ya wakazi wa Moshi wanapohitaji kufanya malipo, kutuma fedha pamoja na huduma zingine za kifedha.

"Pamoja na kuwa na zawadi mbalimbali ambazo zitatolewa kwa watumiaji wazuri wa SimBanking katika kipindi cha promosheni ya 'Benki ni SimBanking', lengo letu kuu ni kufikisha huduma hii kwa kila Mtanzania, jambo ambalo litakwenda kuongeza ujumuishi wa huduma za fedha na kuondoa utamaduni wa kufanya malipo kwa fedha taslimu," alisisitiza Kafui.

Takwimu za robo ya mwisho wa mwaka 2022 za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) zinaonyesha kuwa kuna watumiaji wa simu zaidi ya milioni 58 huku watumiaji wa intaneti wakiwa zaidi ya milioni 31. Ikiwa idadi hiyo yote ikifikiwa na huduma za benki kwa njia ya simu, Tanzania itakuwa imepiga hatua kubwa katika ujumuishaji wa huduma za benki kwa wananchi wake.

Meneja wa Tawi la Benki ya CRDB Moshi, Pamela Mushi, alisema kuwa zawadi zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 565 zitatolewa kwa wateja ambao watafungua akaunti kwa njia ya SimBanking na kufanya miamala mingi zaidi katika kipindi cha promosheni.

"Promosheni ya Benki ni SimBanking inakwenda kuwazawadia wateja wetu ambao ni watumiaji wazuri wa huduma ya SimBanking ambapo fedha taslimu zaidi ya Sh. milioni 350, simu janja 200 sambamba na magari sita (Toyota Crown tano na Toyota Vanguard moja) yanakwenda kutolewa kwa wateja wetu," alisema Pamela.

Promosheni ya Benki ni SimBanking inakuja ikiwa ni kipindi kifupi kimepita baada ya Benki ya CRDB kutangaza taarifa ya fedha ya mwaka 2022 inayoonyesha kuongezeka kwa miamala ya kidigitali ambapo kwa mwaka 2022 zaidi ya asilimia 86 ya miamala ya wateja ilifanywa kwa njia za kidigitali hususan huduma ya SimBanking.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA KUWASILISHA NIA KWA AJILI YA KUSANIFU NA KUTEKELEZA PROGRAMU YA KUFANYA UTAFITI NA KUREJESHA MSITU WA MIKOKO NA ONGEZEKO YAKINIFU LA BIOANUAI YAKE KATIKA BAHARI YA MKOA WA TANGA KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMB NA – REQ-00000157**

Kampuni ya EACOP inazialika kampuni zenye uzoefu na sifa kuwasilisha maombi ya nia ya kutoa huduma ya kuandaa, kusimamia na kutekeleza **''Kusanifu na Kutekeleza Programu ya Kufanya Utafiti na Kurejesha Msitu wa Mikoko na ongezeko yakinifu la bioanuai yake katika Bahari ya Mkoa wa Tanga"** katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP). Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litalofukiwa ardhini, linalokatisha mipaka ya nchi mbili ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi Pwani ya Mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya Kwenda katika Masoko ya Kimataifa. Bomba litaanzia eneo la Kabaale Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, hadi eneo la Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA**

Kituo cha baharini cha Mradi wa EACOP cha Rasi ya Chongoleani kitakuwa na Sehemu iliyo nchikavu ya kuhifadhia mafuta, bandari (njia ya juu ya maji) yenye urefu wa kilomita 2 kuelekea ndani ya bahari, na sehemu ya kupakilia mafuta mwisho wa bandari (njia) hiyo. Katika ujenzi wa njia (bandari) hiyo na matumizi yake sehemu ndogo ya habitati ya Msitu wa Mikoko itaweza kuathiriwa. Mpango wa Utekelezaji wa Bioanuwai (Biodiversity Action Plan) umeshaandaliwa na umeonesha kiwango cha awali cha maeneo yatakayoweza kuathirika. Vifo vya mikoko magondi au mikoko myekundu (Rhizophora mucronate) vimetokea na kuandikwa mwaka 2021 na havihusiani kabisa na shughuli za EACOP.

Inahitajika Kampuni/Taasisi ya kufanya usanifu na utekelezaji wa programu ya urejeshaji wa habitati ya msitu wa mikoko; na kutafiti juu ya sababu zilizopelekea kufa kwa mikoko myekundu katika mdomo wa Mto Zigi, na matokeo ya utafiti huo yatumike katika utekelezaji wa urejeshaji wa mikoko katika Ghuba ya Tanga na kaskazini mwa Tanzania kwa ujumla ikilenga ongezeko halisi (Net Gains) na ikizingatia vigezo na mbinu bora. Njia ya kuyafikia hayo inatakiwa iwe shirikishi ambapo hatua zote zitajumuisha wadau wa ndani na vikundi vyengine, ikiwa ni pamoja na jumuiya za mitaa, taasisi za serikali na mashirika ya kiraia. Maamuzi ya kutekeleza njia au mbinu zitakazokubaliwa yanapaswa kuzingatia takwimu za kisayansi na kuhakikisha ubora wa maamuzi hayo kulingana na hali ya kijamii na mazingira yaliyopo hivi sasa na mwelekeo wa baadae.

**VIGEZO MUHIMU**

Kampuni zinazowasilisha nia zinapaswa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili kama shirika/taasisi ambayo shughuli zake zinahusiana na shughuli za ushirikishaji jamii (kwa mfano urejeshaji wa habitati za baharini unaoshirikisha jamii).
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa kupanga, kusanifu na kutekeleza programu za uendelezaji wa urejeshaji wa misitu ya mikoko, utafiti wa kufa kwa mikoko, kuanzisha vitalu vya miche ya mikoko, kufanya kazi kwa kushirikiana na kujenga uwezo wa jamii za pwani, kufanya utafiti, ufuatiliaji na utengenezaji wa ramani za mtandao wa misitu ya mikoko.
- Mifano ya kazi zinazoonyesha uzoefu wa kufanya kazi zinazofanana na hizo zilizofanywa kipindi cha karibuni, ndani miaka mitano iliyopitaLeseni ya biashara.
- Wasifu wa watendaji watakaohusika katika Mradi ikiwa ni Pamoja na nakala za vyeti vyao, kiwango cha elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma inayohitajika.
- Leseni inayofaa kutoka kwa mamlaka husika ya ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma hii
- Uthibitisho wa Usajili toka Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) au ushahidi thabiti wa maombi ya usajili wakati wa uwasilishaji wa maombi ya nia hii iliyotangazwa.
- Kufuata/kukubaliana na kanuni za Wazawa za Mambo ya Petroli za Tanzania.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni Pamoja na kuwakilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka mfumo wa usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na viwango vya ndani na vya ki-sekta vinayotumika kwa kazi hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za Haki za Binadamu, na kupinga rushwa na ufisadi.

Kampuni zenye nia uwezo na rasilimali ya kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinatakiwa kutuma maombi ya nia yaliyoandaliwa kwa lugha ya Kiingereza pamoja na nyaraka zilizobainishwa hapo juu kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com (ukubwa usiozidi MB20) kabla au si zaidi ya saa 11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe 2nd March 2023.** Kichwa cha cha barua pepe kiwe: [REQ-00000157] _ 'Kusanifu na Kutekeleza Programu ya Kufanya Utafiti na Kurejesha Msitu wa Mikoko na ongezeko yakinifu la bioanuai yake katika Bahari ya Mkoa wa Tanga katika Mradi wa EACOP.

Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.

Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** EACOP itapitia na kuchambua nyaraka ziizotumwa na makampuni yalioonesha nia kulingana na EOI hii, na kisha kufanya tathmini kulighana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila kutoa sababu kwa kampuni husika.

# Wizara: SGR itafungua ajira

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imesema kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutarahisisha maisha ya watu na kuongeza ajira kwa vijana.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Gabriel Migire, wakati wa semina ya kuwajengea uwezo wahariri wa vyombo vya habari.

Alisema mpaka sasa zaidi ya Watanzania 20,000 wameajiriwa kwenye mradi huo katika nafasi mbalimbali na hali iliyosababisha kupunguza wimbi la vijana waliokuwa mtaani kwa kisingizio cha kukosa ajira.

Aidha, alibainisha kuwa mradi huo utainua uchumi wa nchi kwa kasi, akisisitiza utamwezesha mtu kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa haraka zaidi tofauti na gari.

"Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imepewa asilimia 9.3 ya bajeti nzima ya serikali ya mwaka ambayo ni takribani Sh. trilioni nne kila mwaka, hii inaonyesha jinsi gani sekta hii ilivyo nyeti, na muhimu kwa taifa hili, mfanyabiashara anaweza kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma kwa saa tatu, haya ni maendeleo makubwa.

"Tutaendela kutoa ajira kwa sababu mradi huu unahitaji rasilimali watu, hivyo niwatake Watanzania kuchangamkia fursa zinapotangazwa kuhusu mradi huu," alisema.

Aliongeza kuwa mradi huo pia utasaidia kuvutia wawekezaji kwa kuwa wawekezaji wengi huzingatia kuwapo mazingira mazuri ya usafirishaji.

"Wafanyabiashara na wawekezaji wakubwa wanaangalia miundombinu iliyopo kwenye nchi fulani, ili waweze kuwekeza. Kwa hiyo, utakapokamilika mradi huu, utafungua fursa kwa wawekezaji kwa kiasi kikubwa," alisema.

Kiongozi huyo pia aliwataka wahariri hao kujiepusha kutoa taarifa zenye nia ovu na mradi, akiwaomba kujenga utamaduni wa kujiridhisha kutoka kwenye vyanzo husika.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, alisema ujenzi wa reli hiyo ni matokeo ya juhudi za marais kuhakikisha uchumi wa nchi unakua na kuongeza pato, pia kuiunganisha Tanzania na nchi jirani hasa za ukanda wa magharibi zenye malighafi nyingi.

Msemaji Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi Idara ya Habari Maelezo, Gerson Msigwa, aliwataka wafanyakazi wa TRC kuepuka urasimu pindi wanapotafutwa na waandishi wa habari kwa lengo la kupata taarifa.

"Tutoe ushirikiano kwa waandishi wa habari, wakati mwingine upotoshaji unatokea pale chanzo cha habari unaposhindwa kutoa ushirikiano kwa sababu mwisho wa siku mwandishi atataka habari yake itoke.




Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Absa Tanzania, Abdi Mohamed (kulia), wakishuhudia Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Nehemia Mchechu, akitia saini makubaliano yatakayowawezesha wateja wa Absa kununua nyumba za NHC kwa mkopo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Raia China kizimbani mashtaka kuisababishia hasara serikali

**Na Grace Gurisha**

RAIA wa China Li Naiyong amepandishwa kizimbani kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam akikabiliwa na mashtaka ya uhujumu uchumi, akidaiwa kuisababishia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) hasara ya Sh. milioni 221.1.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Yusuph Aboud alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Pamela Mazengo kuwa mshtakiwa anakabiliwa na mashtaka sita ya uhujumu uchumi.

Alidai kuwa kati ya Agosti 13 hadi Oktoba 22, 2022, kwenye Hoteli ya Hongkong iliyoko Kariakoo, Ilala jijini Dar es Salaam, raia huyo aliingiza vifaa mbalimbali vya mawasiliano vya kielektroniki bila kuwa na leseni.

Ilidaiwa kuwa katika tarehe hizo, mshtakiwa huyo alisimika na kusimamia mitambo ya mawasiliano ya kielekroniki bila kuwa na leseni kutoka TCRA.

Alidai katika tarehe hizo, mshtakiwa huyo kwa nia ovu, alitumia mawasiliano kwa kutumia vifaa hivyo vilivyounganishwa katika njia ya mawasiliano kwa lengo la kupokea na kutoa mawasiliano bila ya kuwa na leseni.

Mshtakiwa huyo pia anatuhumiwa kuendesha mitambo hiyo kwa lengo la kupokea na kusambaza mawasiliano kimataifa na kufanya matumizi mabaya ya vifaa hivyo kwa nia ya kukwepa makato kwa kupokea na kusambaza simu za kimataifa bila leseni.

Mshtakiwa huyo pia anadaiwa katika tarehe hizo, kwa vitendo vyake hivyo, aliisababishia serikali na TCRA hasara ya Sh. 221,163,600.

Baada ya kusomwa mashtaka hayo, upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo unaendelea, hivyo kesi hiyo iliahirishwa hadi Machi Mosi, 2023 kwa ajili ya kutajwa.

Mshtakiwa huyo alipelekwa mahabusu baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana, ikiwamo kuwasilisha mahakamani hati ya mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. 110,581,800 na wadhamini wawili mmoja kati ya hao awe mtumishi wa serikali.

## Mshtakiwa kesi kocha wa Simba aomba upelelezi ukamilike aone wanawe

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA Sarah Eliud anayeshtakiwa pamoja na aliyekuwa Kocha wa Makipa wa Klabu ya Simba, Mwalami Sultan kwa tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya, ameiomba mahakama kuharakisha upelelezi wa kesi inayowakabili kwa kuwa amekaa gerezani na hajui maendeleo ya wanawe.

Mbali na Sultan na Eliud, washtakiwa wengine ni Mmiliki wa Kituo cha Kambiasso Sports Academy, Kambi Seif, Maulid Mzungu, Said Matwiko, John John na Sarah Eliud.

Eliud aliwasilisha ombi hilo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi.

Alidai kuwa yeye yupo gerezani na hajui watoto wake wanaendeleaje na wanalelewaje, hivyo anaomba upande wa mashtaka waharakishe kukamilika kwa upelelezi.

Baada ya kudai hivyo, Hakimu Mrio alimuuliza kama hana ndugu wanaokwenda kumtembelea gerezani na kumpatia taarifa za maendeleo ya watoto wake.

Akijibu suala hilo, Eliud alidai wapo ndugu ambao wanakwenda kumtembelea, lakini hajui watoto wake wanalelewa katika mazingira gani.

"Basi vumilia hadi upelelezi utakapokamilika," alisema Hakimu Mrio.

Awali Wakili wa Serikali, Caroline Matemu, alidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na aliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Machi 2 mwaka huu kwa ajili ya kutajwa. Washtakiwa hao wanatuhumiwa kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin kilo 34.89.

Ilidaiwa kuwa Oktoba 27, 2022, huko Kivule, ndani ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, washtakiwa walikutwa wakisafirisha kilo 27.1 za dawa za kulevya aina ya heroin.





# Ongezeko matukio ya ukatili wa kingono lawaibua wadau

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

ONGEZEKO la kesi za matukio ya ukatili wa kingono na kimwili katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, limewaibua wadau wa haki za binadamu ambao wameitisha jukwaa la pamoja la kujadili mustakabali wa baadaye wa wanawake na watoto.

Kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka 2022 katika Manispaa hiyo, kuliripotiwa matukio 1,703 ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Akieleza jana namna hali ilivyo kwa sasa, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Manispaa ya Moshi, Magreth Reuben, alisema kata zilizoathirika zaidi ni Miembeni, Kaloleni na Njoro, ambako kuna maeneo yanayotuhumiwa kuonyesha picha za video (vibanda umiza), mipira na vituo vidogo vya kucheza kucheza watoto.

"Ukatili wa kingono kwa watoto, sasa hivi umekuwa ukishamiri katika maeneo mengi, kikao hiki kitakuja na Mpango Kazi wa Taifa wa Kupambana na Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) unaounga kupunguza au kutokomeza ukatili nchini.

Alisema maelezi ndiyo kichochezi kikubwa kinachochochea uwepo kwa ukatili wa kijisia hususani wa kingono.

"Tunaona kwamba hata ukatili wa kimwili, matukio yaliyoripotiwa 315, ukatili wa kingono 168 na ukatili wa kisaikolojia yalikuwa matukio yanayowahusu wanawake 593 na wanaume 109,"alisema.

Mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa Wilaya ya Babati (Manyara), alieleza kukerwa na ongezeko la matukio hayo ya ukatili wa kingono nchini, akisema amepokea ripoti inayoonyesha kuwa kesi za ukatili wa kingono dhidi ya watoto zilikuwa 708 na ukatili wa kimwili 792.

Ofisa Mipango wa Shirika la Simba Footprint, Belinda Urio, akizungumzia lengo la kuitisha jukwaa hilo, alisema ili kukabiliana na ongezeko hilo, Simba Footprint, limewakutanisha walimu na maofisa watendaji wa mitaa na kata, kujadili athari za kiafya, kisaikolojia na hatua ambazo zinapaswa kuchukuliwa.

Aidha, Mkuu wa Dawati la Jinsia la Watoto na Wazee, Wilaya ya Moshi, Mkaguzi wa Polisi, Nsangarufu Mwaipopo, alisema kutokana na wimbi kubwa la ukatili wa kijinsia linaloendelea, wamegundua linachochewa na tatizo kubwa la makosa ya kimaadili.

"Makosa hayo yanahusiana na wananchi kujichukulia sheria mkononi na ukifuatilia kisa ni wivu wa mapenzi au ni hali inayotokana na imani za kishirikina,"alisisitiza.

Mmoja wa wanufaika wa programu hiyo, ambaye ni Mwenyekiti wa Dawati la Kata ya Miembeni, Agnes Kambi, amesema matukio ya ukatili wa jinsia kama ubakaji, ulawiti, vipigo, saikolojia na ukatili wa kiuchumi, hutokea.

# Vigogo AMCOS wamtunishia msuli mrajis, wagoma kung'oka

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

VIONGOZI watano wa juu wa Bodi ya Chama cha Msingi cha Ushirika wa Mazao cha Masama Roo AMCOS, kilichoko Wilaya ya Hai, wamegomea uamuzi wa Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Kilimanjaro, Jacquiline Senzige wa kuwang'oa madarakani wakidai amekanyaga katiba.

Mrajis huyo alifikia uamuzi huo akidai kuwa bodi hiyo imemaliza muda wake kwa mujibu wa sheria za vyama vya ushirika.

Akizungumzia mgomo huo jana, Mwenyekiti wa bodi hiyo, Patrick Munisi, alisema hawatakabidhi ofisi ya chama hicho kama alivyoagiza Senzige, kwa kuwa ajenda ya kikao hicho haikuwa mkutano maalum wa kusoma ripoti ya ukaguzi, isipokuwa ulikuwa wa kusoma mapato na matumizi.

Alisema kilichofanywa na Mrajisi, Februari 8 mwaka huu ni haramu, kwa kuwa aliagiza kuitishwa mkutano maalum wa kusoma mapato na matumizi, kuanzia mwaka 2018 hadi 2022, na siyo mkutano uliotokana na ripoti ya ukaguzi, ambayo inampa mamlaka ya kufanya alichokifanya.

"Baada ya kuamuru hivyo, kulitokea mzozo mkubwa wa kutoelewana baina ya Mrajis na wanachama na baadaye tukafikia hatua ya kupiga kura za kuondolewa,"alisema.

Aliongeza kuwa wanachama walikuwa 110 wajumbe walipigakura kutokuwa na imani na bodi ni 37 na walitaka bodi iendelee ni 75.

Alisema baada ya kura hizo Mrajis Msaidizi alikataa bodi hiyo kuendelea kuwa madarakani, hivyo kuamuru wajumbe wapendekeze bodi ya mpito hadi hapo uchunguzi utakapofanyika.

Kiini cha mgogoro huo kitajwa kuwa ni wajumbe wa bodi kugawanyika juu ya ukodishaji wa shamba la Kibo na Kikafu, lenye ukubwa wa ekari 2,054 ambalo lilikuwa na mgogoro wa muda mrefu na mwekezaji aliyekuwapo awali.

Kwa mujibu wa Munisi wakati wanaendelea na mchakato wa kutafuta mwekezaji mpya wa shamba hilo, wajumbe wa bodi akiwamo Mwenyekiti na mjumbe mmoja walipelekwa Nairobi nchini Kenya, kutembelea Kiwanda cha Kampuni ya Avoafrica kinachomilikiwa na mwekezaji huyo aliyeomba zabuni ya kuliendesha shamba hilo.

Alisema katika safari hiyo, walikwenda wajumbe saba wanaotokana na vyama vinne vinavyosimamia shamba hilo, Mrajis Msaidizi na Mbunge wa Hai, Saashisha Mafuwe ili washawishi kupitishwa zabuni hiyo.

Inaelezwa kuwa mwekezaji huyo hakupata zabuni hiyo na bahati iliangukia kwa mwekezaji mwingine wa Kampumi ya MACJARO.

Alisema mwekezaji huyo wa Kenya, ambaye anadaiwa hakuwa na vigezo, alitaka alime parachichi, lakini aliyeteuliwa amekubali kulima kahawa, parachichi na karanga mti (makademia).

Alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhusu madai hayo, Mrajis Msaidizi wa mkoa wa Kilimanjaro, Jacquline Senzige, alisema kuondolewa kwa bodi hilyo ni takwa la kisheria, kwa kuwa muda wao wa kukaa madarakani umeisha.

Kuhusu madai ya kupelekwa Kenya, alisema yeye hawezi kuzumgumzia suala hilo, na kwamba mchakato wa kumpata mwekezaji katika Shamba la Kibo na Kikafu, umesitishwa na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Tanzania Dk. Benson Ndiege, ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC).



Mkurugenzi wa Tiba na Uokoaji wa Kampuni ya KILIMEDAIR, Dk. Hussein Abradha (katikati), akimwokoa mgeni aliyepata changamoto ya hali ya hewa kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro kwa kumpakia kwenye helikopta ili kuwahi matibabu. **PICHA: JAMES LANKA**

# Operesheni rejesha mtoto shule yanasa watoto 50

**Na Dege Masoli,** KILINDI

OPERESHENI rejesha mtoto shuleni inayoendeshwa na Ofisa Tarafa ya Kwekivu, Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga, Michael John imewatia mbaroni watoto 50 walikuwa wakitumikishwa katika mgodi wa dhahabu wa Lundamila Seita Kata ya Pagwi.

Akizungumza na Nipashe, John alieleza kuwa operesheni hiyo sambamba na watoto hao wengine waliyokamatwa ni pamoja na wazazi wao.

Alieleza kuwa kamata kamata hiyo ni ya kata zote nane za tarafa hiyo na lengo ni kuhakikisha kila mtoto anayestahili kwenda shule anakuwa darasani sambamba na waliotakiwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu.

Aidha, alieleza kuwa zoezi hilo limeanza maeneo ya migodini ambako inasemekana watoto hao wamekimbilia kufanyakazi mbalimbali zikiwamo biashara na kutumikishwa kuchota maji na kazi kwenye migahawa ya vyakula.

Ofisa Kata ya Pagwi, Abdalah Mngoya, alielezea zoezi hilo kuwa ni la siku saba na linahusisha vijiji vyote saba ambavyo ni Chamtui, Pagwi, Lumotio, Nyamaleni, Mtakuja Makelele na Masilei.

"Tumeanza leo katika machimbo ya dhahabu ya hapa Lundamila Seita na tumewakamata watoto waliokuwa katika mazingira hatarishi wapatao 40 wakiwamo na wazazi wao na wengine 13 ni wa mitaani, sasa tunafanya mpango wa kuwafikisha shule," alieleza Mngoya.



# Mbarawa ahimiza ushirikiano ujenzi barabara ya kimataifa

**Na Titus Mwombeki,** NGARA

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amewaelekeza viongozi wa Mkoa wa Kagera kufanya kazi kwa ukaribu na mkandarasi wa Kampuni ya China Engineering Construction Company aliyekabidhiwa tenda ya ujenzi wa Barabara ya Lusaunga Rusumo ili ikamilike kwa wakati.

Barabara hiyo inaziunganisha nchi ya Tanzania, Rwanda, Burundi na Uganda.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki baada ya kushuhudia utiaji saini wa ujenzi wa barabara hiyo baina Kampuni ya China Engreering Construction Company na Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS).

**Barabara ina urefu wa kilometa 92 na itagharimu zaidi ya Sh. bilioni 152 na ujenzi wake unategemewa kukamilika ndani ya miaka miwili.**

"Nawaomba viongozi mshirikiane na mkandarasi aliyekabidhiwa tenda ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami ili kuhakikisha anamaliza kazi hii kwa muda uliokusudiwa."

Aidha, aliwaomba wananchi wa Mkoa wa Kagera kuwa wakalimu na kujiepusha na tabia ovu ikiwa ni pamoja na wizi wa vifaa vya ujenzi suala ambalo linaweza kusababisha ujenzi wa barabara hiyo usikamilike kwa muda kusudiwa.

Naye Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchi TANROADS, Mhandisi Rogatus Mativila, akisoma taarifa za mradi alisema kuwa barabara hiyo ina urefu wa kilometa 92 na itagharimu zaidi ya Sh. bilioni 152 na ujenzi wake unategemewa kukamilika ndani ya miaka miwili.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, akizungumza katika hafla hiyo alisema serikali imedhamilia kufungua Mkoa wa Kagera kiuchumi, huku akiwataka wananchi wa Mkoa huo kufanya kazi kwa bidii na kuongeza uzalishaji.




Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Rogatus Mativila, akisaini mkataba na wawakilishi wa China Engineering Construction Company wa ujenzi wa barabara ya Lusaunga Rusumo kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 92 inayotarajiwa kugharimu Sh. bilioni 152 na kuunganisha nchi ya Tanzania, Uganda, Rwanda na Burundi. **PICHA: TITUS MWOMBEKI**

# Wachimbaji wadogo madini wachangia ushuru bilioni 3.5/-

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WACHIMBAJI wadogo katika mgodi mdogo wa Chapakazi ulioko Kijiji cha Mwongozo, Kitongoji cha Nyandolwa, Kata ya Mwenge Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, wamechangia ushuru wa Sh. bilioni 3.5 kutokana na shughuli wanazozifanya mgodini hapo.

Ushuru huo ulikusanywa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22 wakishika nafasi ya tatu kitaifa katika makusanyo hayo.

Mwenyekiti wa mgodi huo, Joshua Sayi, aliyabainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya namna wanavyodhibiti utoroshaji wa mawe yanayosadikiwa kuwa na madini ya dhahabu.

Alisema wamechangia ushuru wa huduma serikalini kiasi cha Sh. bilioni 3.5 kati ya hizo kiasi cha Sh.bilioni 1.6 kimechangiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga na serikali kuu Sh.bilioni 1.9.

Sayi alisema ulipaji mzuri wa mapato ya serikali umechangiwa na ushirikiano mkubwa baina ya uongozi wa mgodi huo na halmashauri hali ambayo mpaka sasa wamekuwa na maendeleo mazuri katika uzalishaji wa dhahabu katika Mkoa wa Shinyanga.

Alisema hadi sasa wametoa ajira 600 kwa wananchi wanaowazunguka.

Meneja wa mgodi huo, Abduly Musa, alisema eneo hilo walikabidhiwa na Rais Samia Suluhu Hassan tangu mwaka 2021 na kudai tangu wakati huo wamekuwa wakifanya vizuri katika uzalishaji na ulipaji wa mapato ya serikali kwa wakati bila mvutano wowote.

Alisema katika suala la usalama mgodini hapo wameliweka kipaumbele kwa kuhakikisha kuwa mashimo yote ambayo yanachimbwa na kukosekana dhahabu yanafukiwa kwa wakati.

Katibu wa mgodi huo, Peter Jonathani, alisema mbali na kuendesha shughuli za kiuchimbaji pia wamekuwa wakishiriki katika shughuli za maendeleo katika kijiji hicho ikiwa ni pamoja na kujenga madarasa matatu katika Shule ya Msingi Nyandolwa na sita katika Shule ya Sekondari Gembe.

# Mwalimu aeleza faida za umeme wa REA shuleni

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Isunda iliyopo Itilima wilayani Kishapu, Viola Shuma, amesema upatikanaji wa huduma ya umeme shuleni hapo imesaidia nyaraka za siri za serikali kuwa salama, pamoja na mitihani ya majaribio ya wanafunzi kutovuja.

Shule hiyo ya Msingi Isunda ni miongoni mwa taasisi za serikali ambazo zimeunganishiwa huduma ya umeme wa REA wilayani Kishapu.

Mwalimu Shuma alibainisha hayo juzi wakati wa uzinduzi wa kuwasha umeme huo katika vijiji vitatu wilayani Kishapu, ambavyo ni Itilima, Ikonokelo na Ipeja.

Alisema kabla ya kuwapo kwa nishati ya umeme shuleni hapo, walikuwa wakipata huduma ya mtandao kwenye 'stationary' za watu binafsi pamoja na kuchapa mitihani ya majaribio ya wanafunzi sehemu ambazo siyo salama hali iliyokuwa ikisababisha kuvuja kwa mitihani shuleni.

"Tunashukuru kupata huduma ya umeme hapa shuleni sasa hivi nyaraka za serikali zitakuwa salama zaidi, sababu kwenda kufungua email kwenye stationary za watu binafsi ni hatari sana, lakini sasa hivi tutanunua vitendea kazi ili huduma zote zifanyike hapa hapa shule na mitihani itakuwa salama pia,"alisema Shuma.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Itilima Mwakwaiya Mwandu, alisema umeme kufika kijijini humo kutachochea ukuaji wa uchumi, sababu wananchi wataanzisha miradi ya kiuchumi zikiwamo mashine za kusaga nafaka, viwanda vidogo na huduma za uchomeleaji na vijana kupata ajira.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, aliwataka wananchi wilayani humo ambao tayari vijiji vyao vimefikiwa na umeme wafanye utaratibu wa kulipa TANESCO ili waunganishiwe umeme majumbani mwao na maeneo yao ya biashara, huku akiwapa tahadhari ya kutowatumia vishoka.

Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo, aliwasihi wananchi jimboni humo kutohujumu mradi huo wa umeme wa REA, ikiwa ni pamoja na kuiba vifaa vya ujenzi.

Hivyo, aliwataka kila mmoja awe mlinzi wa mwenzake, sababu upatikanaji wa nishati ya umeme vijijini ni kichocheo kikubwa cha maendeleo.

**Umeme kufika kijijini humo kutachochea ukuaji wa uchumi, sababu wananchi wataanzisha miradi ya kiuchumi zikiwamo mashine za kusaga nafaka, viwanda vidogo na huduma za uchomeleaji na vijana kupata ajira.**

# Nipashe Spotika




MAGWIJI WA5 WATAKAOKUWA HURU MWISHONI MWA MSIMU 12 - 13



# VIUNGO WA4 WABUNIFU BORA EPL KWA SASA

**LONDON, England**

LIGI Kuu England (EPL), imetoa baadhi ya wachezaji wabunifu wa safu ya kiungo katika soka kwa miaka mingi. Baadhi yao ni pamoja na Cesc Fabregas, David Silva, Juan Mata, Mesut Ozil na Santi Cazorla.

Kuwa na viungo wabunifu ni bonasi kubwa kwa kila timu. Wanasaidia katika kufungua safu ngumu zaidi za ulinzi na kutengeneza nafasi kwa wenzao.

Msimu unaoendelea wa Ligi Kuu England 2022-23, hauna upungufu wa wachezaji kama hao. Hivyo makala haya inawaangalia viungo wanne bora wabunifu zaidi katika ligi hiyo kwa sasa...

**#4. Bernardo Silva - Manchester City**

Wachezaji wachache sana katika Ligi ya England wanaweza kumshinda nyota wa Ureno na mchezaji wa Manchester City, Bernardo Silva katika suala la ufundi wa pande zote.

Kiungo huyo ameendelea kuwa mmoja wa viungo bora wa ligi tangu aliposajiliwa kwa kitita cha euro milioni 50 kutoka AS Monaco kwenda Manchester City mwaka 2017.

Ingawa Silva anajulikana sana kwa kiwango chake cha juu cha kazi na ustadi, Mreno huyo pia ana uwezo wa ajabu wa ubunifu.

Kiungo huyo wa kati wa Ureno hadi sasa anashika nafasi ya pili kwa asisti nyingi zaidi kwa kikosi cha Pep Guardiola msimu huu, nyuma ya Kevin de Bruyne, ambaye ana asisti tisa. Silva pia yuko katika nafasi ya nne katika chati ya pasi za mabao kwenye ligi, akiwa nazo tano.

**#3. Martin Odegaard**

Nahodha huyu wa Arsenal amekomaa taratibu na kuwa mmoja wa viungo wabunifu wa Ligi Kuu England, kulingana na kiwango chake msimu huu.

Martin Odegaard amekuwa kiungo muhimu wa timu ya vijana ya Mikel Arteta ambao wamekuwa moto kwenye ligi.

Nyota huyo wa Hispania ameweza kuboresha kiwango chake na kuwa mchezaji wa aina ya Mesut Ozil kutokana na uwezo wake wa kuona na kupiga pasi.

Amekuwa mchezaji aliyechangia mabao mengi zaidi kuliko mchezaji yeyote wa Arsenal kwenye ligi msimu huu baada ya kufunga mabao saba na kutoa asisti tano.

Odegaard pia yuko katika nafasi ya nne kwenye chati ya pasi za mabao katika ligi msimu huu, akiwa nazo tano. Pia alitawazwa Mchezaji Bora wa Ligi wa Desemba.

#2. Christian Eriksen

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Denmark bila shaka ni mmoja wa wachezaji waliofanya vema katika usajili wa majira ya joto katika Ligi Kuu England msimu huu. Alijiunga na Manchester United baada ya kumalizika kwa mkataba wake kule Brentford.

Christian Eriksen amekuwa na mchango mkubwa kwa 'Mashetani Wekundu' hao kwani kwa sasa wako kwenye kinyang'anyiro cha kuwania mataji manne.

Kipengele kimoja cha mchezo wa Eriksen ambacho kimejitokeza katika msimu huu unaoendelea ni ubunifu wake. Kiungo huyo wa Denmark kwa sasa anajivunia kutoa pasi nyingi za mabao kuliko mchezaji yeyote wa Mashetani Wekundu kwenye mashindano yote (nane).

Pia kwa sasa anashika nafasi ya pili kwa asisti nyingi kwenye ligi (6), nyuma ya kiungo wa Manchester City, De Bruyne (9).

**#1. Kevin de Bruyne - Manchester City**

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Ubelgiji anaendelea kuonyesha kiwango chake na kuthibitisha thamani yake kama mmoja wa viungo bora zaidi duniani.


De Bruyne anajulikana kwa uoni wake mzuri wa mpira na hivyo kumfanya aandikishe pasi nyingi za mabao katika maisha yake yote ya soka.

Kwa upande wa ubunifu, ni wachezaji wachache sana wanaoweza kushindana na nyota huyo wa Manchester City kwenye Ligi Kuu. Kiungo huyo kwa sasa anaongoza katika orodha ya watoa pasi za mabao kwenye ligi akiwa nazo tisa.

De Bruyne pia ana pasi 14 za mabao kwa jumla katika mashindano yote, jambo ambalo linamfanya kuwa mtoa pasi nyingi zaidi kwa timu ya Guardiola.

## ISIKUPITE

CRISTIANO Ronaldo ndiye mchezaji mwenye wafuasi wengi zaidi (milioni 813.5) kwenye mitandao ya kijamii akifuatiwa na Lionel Messi (milioni 541), Neymar Jr. (milioni 385), Kylian Mbappe (milioni 125.9) na Marcelo Vieira (milioni 115.6).



# MAGWIJI WA5 WATAKAOKUWA HURU MWISHONI MWA MSIMU

**LONDON,** England

MWISHO wa msimu wa soka ni wakati wa msisimko mkubwa kwa timu zote za soka. Pia ni wakati wa kufanya tathmini ya wachezaji waliopo na wale ambao wataruhusiwa kuondoka klabuni bure.

Kila mwaka, kuna wachezaji wachache ambao wanakuwa huru. Baadhi yao wamekuwa nyota katika timu zao, huku wengine wakiwa bado hawajajiimarisha kama washindi kwenye vikosi vyao.

Makala haya yanawaangalia wanasoka watano ambao wamethibitisha ustadi wao mara kwa mara. Uzoefu wao na ustadi wao umewafanya kuwa wa thamani kwa timu zao, lakini wamepangwa kuwa wachezaji huru.

Hawa ni magwiji watano wa soka ambao mikataba yao itamalizika mwishoni mwa msimu huu...

**#5. Marco Reus**

Nahodha wa Borussia Dortmund anayekabiliwa na majeraha, Marco Reus yuko katika miezi ya mwisho ya mkataba wake kule Signal Iduna Park. Winga huyo amekuwa mtumishi mwaminifu kwa klabu hiyo tangu ajiunge nayo akitokea Borussia Monchengladbach mwaka 2012, akikataa kuhamia Bayern Munich.

Reus amechangia kwa mabao manne na asisti tatu katika mechi 15 alizoichezea klabu hiyo msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, amekuwa na wakati mgumu na majeraha katika maisha yake ya soka, na kukaa nje kwa muda mrefu. Reus anasemekana kuangaliwa na klabu kadhaa za Mashariki ya Kati, pamoja na Al-Nassr ya Saudi Arabia.

Reus ameichezea Borussia Dortmund zaidi ya mechi 300 katika miaka yake 11 katika klabu hiyo. Winga huyo sasa anaweza kuchukuliwa kuwa ni ziada kwa mahitaji katika klabu na anaweza kuwa njiani kuondoka kama mchezaji huru Julai mwaka huu.

**#4. N'Golo Kante**

Baada ya miaka saba Chelsea, huenda ukawa wakati wa N'Golo Kante kuiaga klabu hiyo. Kiungo huyo wa kati wa Ufaransa, aliimarisha nafasi yake kama mmoja wa wachezaji bora zaidi ulimwenguni katika nafasi yake wakati akiwa Stamford Bridge. Hata hivyo, Kante amekuwa na wakati mgumu kubaki fiti katika misimu ya hivi karibuni akiwa Chelsea na hajaichezea klabu hiyo tangu Agosti mwaka jana.

Kante alishinda taji la Ligi Kuu England akiwa na Chelsea katika msimu wake wa kwanza na klabu hiyo na pia ameisaidia kunyanyua Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Umiliki mpya wa Chelsea unaonekana kujenga timu ya soka ya vijana wenye vipaji na Kante akiwa na umri wa miaka 31, hawezi kuonekana kuwa kijana. Mazungumzo juu ya mkataba mpya yamekwama.

Kante bado anafanya kazi ya kurejea Stamford Bridge kabla ya uamuzi wake kuhusu hatima yake kufikiwa. Pande zote mbili zinasemekana kuunga mkono kuendelea na uhusiano wao ikiwa tu masharti sahihi yatatimizwa. Kiungo kama Kante atakuwa na klabu nyingi zitakazomwania kama mchezaji huru.

**#3. Luka Modric**

Mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or mwaka 2018 na kiungo wa kati wa Real Madrid, Luka Modric yuko katika tafrija ya maisha yake ya soka. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, mkataba wake Santiago Bernabeu unamalizika Juni mwaka huu na hakuna dalili zozote za kuongeza muda wake wa kubaki katika klabu hiyo. Modric anasalia kuwa miongoni mwa viungo bora zaidi duniani licha ya umri wake.

Licha ya umri wake, Modric ameichezea Real Madrid mara 26 msimu huu katika michuano yote. Kiungo huyo mkongwe amekuwa katika klabu hiyo tangu mwaka 2012 na amepata mafanikio makubwa klabuni hapo. Modric alitia saini mkataba mpya katika klabu hiyo mwaka 2020 baada ya kudaiwa kuhamia Inter Milan. Kiungo huyo sasa anaweza kuchukuliwa kuwa amepita kiwango chake bora na huenda asipewe nafasi ya kuongezwa tena.

Real Madrid wameripotiwa kumtaka Modric kustaafu soka la kimataifa ikiwa ana nia ya kuendelea kuitumikia klabu hiyo. Nahodha huyo wa Croatia, Modric alitangaza nia yake ya kuendelea na timu ya taifa baada ya kumaliza katika nafasi ya tatu nchini Qatar. Katika miezi ijayo, Real Madrid na Modric wataamua iwapo wataendelea pamoja au kuachana.

**#2. Karim Benzema**

Mshambuliaji wa zamani wa Ufaransa, Karim Benzema aliandika jina lake kwenye vitabu vya historia aliposhinda tuzo ya Ballon d'Or mwaka 2022. Nahodha huyo wa Real Madrid amekuwa na maisha mazuri katika klabu hiyo, lakini wakati wake unaweza kuwa unakaribia mwisho. Amepambana na majeraha msimu huu, akicheza mechi 19 pekee na kufunga mabao 12.

Benzema alijiunga na Real Madrid mwaka 2009 na amewashinda Gonzalo Higuain, Alvaro Morata na Luka Jovic ili kusalia kuwa muhimu katika klabu hiyo. Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 35, amepata hadhi ya kuwa maarufu Santiago Bernabeu na huenda anatafuta kuondoka katika klabu hiyo. Amecheza soka lake bora katika rangi za 'Los Blancos' hao.

Real Madrid walitumia euro milioni 60 kumsajili kinda wa miaka 16 kutoka Brazil, Endrick kutoka Palmeiras. Mshambuliaji huyo ambaye atajiunga na klabu hiyo atakapofikisha umri wa miaka 18, anaonekana kuwa mbadala wa muda mrefu wa Benzema. Miezi ijayo itakuwa muhimu katika kutoa ufafanuzi wa wazi wa mipango ya klabu kwa Benzema.

**#1. Lionel Messi**

Lionel Messi alisaini mkataba wa miaka miwili kujiunga na Paris Saint-Germain kutoka Barcelona mwaka 2021. Nyota huyo wa soka wa Argentina amefurahia muda wake wa kukaa Paris, lakini anaonekana kuwa na wasiwasi kuhusu kuongeza mkataba wake katika klabu hiyo. Aliiongoza nchi yake kwa mafanikio kushinda Kombe la Dunia la mwaka 2022 na uvumi umeenea juu ya mustakabali wake.

Messi amekuwa mmoja wa wachezaji waliochangia vema PSG msimu huu, akiwa amefunga mabao 10 na kutoa pasi za mabao 10 kwenye Ligue 1. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, anasemekana kuwa ametulia kuhusu hali ya mkataba wake klabuni hapo, lakini hakuna dalili zozote kama atasaini.

Tangu Kombe la Dunia, imekuwa ikikisiwa sana kwamba amepokea ofa kutoka kwa David Beckham anayemiliki klabu ya Inter Miami inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani, MLS. Kurejea Barcelona pia kumekuwa na uvumi, ingawa anasemekana kutokuwa na maelewano mazuri na rais, Joan Laporta.

Messi amewahi kuchezea klabu mbili tu katika maisha yake ya soka. Kuna uwezekano kwamba atarejea Argentina kuchezea Newell's Old Boys, klabu yake ya utotoni, mwishoni mwa maisha yake ya soka. Mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or ana miezi michache kuamua ni wapi anakusudia kutumia maisha yake ya baadaye.


BENZEMA

## Nukuu

"Kufanya mazoezi na Messi [Lionel] yaliniacha mdomo wazi. Nilikuwa nikisema kwamba Cristiano Ronaldo alikuwa bora zaidi duniani, lakini Messi ni kitu kingine. Yeye si wa kawaida. Nilijiona sitoshelezi kwa mara ya kwanza katika taaluma yangu. Alikuwa akifanya mambo ya ajabu. Nilihisi kusema, 'Nimemaliza, nitaacha kucheza!'" **Kiungo wa zamani wa Barcelona, Kevin-Prince Boateng akielezea nyakati zake akiwa Camp Nou na Messi.**



"Nina uhusiano mzuri na Cristiano, chaguo lake ni zuri na linafaa, Saudi Arabia itafurahia mchezaji bora ambaye ana kipaji kikubwa na mchezaji mzuri wa kulipwa," **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti kuhusu Ronaldo kujiunga na Al-Nassr**



"Mpango wetu wa mchezo, bila shaka, ubora kweli na uwanjani wanapaswa kuchukua uamuzi. Aliamua katika hatua ya mwisho kwenda kwenye kona kushambulia, lakini siipendi. Lakini sikumwambia chochote, kabla au baada ya hapo kwa sababu katika maisha yangu yote ya soka sijawahi kuwaambia makipa wetu wafanye hivyo na kitakwimu zinaenda kinyume na timu na kipa kufunga bao lolote," **Unai Emery baada ya uamuzi kipa Emi Martinez kwenda kushambulia mpira wa kona na Arsenal kufanya shambulizi la kushtukiza na kufunga bao la nne dhidi ya Aston Villa juzi.**



# SABABU 5 SIMBA KICHAPO KWA MKAPA DHIDI YA RAJA



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza (kulia), akijaribu kupenyeza mpira dhidi ya beki wa Raja Casablanca, Mohamed Al Makahasi, katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika juzi iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, wenyeji wakipoteza kwa mabao 3-0.

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza Simba imepoteza mechi yake ya kwanza dhidi ya timu za Afrika Kaskazini, maarufu kama 'timu za Waarabu' nchini, ilipofungwa mabao 3-0 dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco.

Juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ilichapwa mabao 3-0 dhidi ya timu hiyo, ikiwa ni mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kutibua rekodi yao hiyo.

Yalikuwa ni mabao ya Hamza Khabba dakika ya 30, Soufiane Benjdida aliyefunga dakika ya 82 na Ismael Mokadem aliyepachika kwa mkwaju wa penalti dakika ya 86.

Raja Casablanca inakuwa timu ya kwanza ya 'Waarabu,' kuifunga Simba kwenye ardhi ya nyumbani, ikicheza nayo pia kwa mara ya kwanza kwenye historia za timu hizo.

Pia inakuwa timu ya nne kuifunga Simba kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ambapo Aprili 3, 2011 ilifungwa mabao 3-2 dhidi ya TP Mazembe, Februari 17, 2013 ilifungwa na Recreativo de Libolo ya Angola bao 1-0 na Oktoba 24, 2021 ilichapwa mabao 3-1 dhidi ya Jwaneng Galaxy, huku mechi zote hizo zikiwa ni za Ligi ya Mabingwa Afrika. Dhidi ya Libolo, TP Mazembe na Jwaneng Galaxy zilikuwa ni za mechi za Raundi ya Kwanza, huku ya juzi ilikuwa ni hatua ya makundi.

Hata hivyo, bado Simba ndiyo timu iliyoshinda mara nyingi zaidi kwenye uwanja huo kwenye mechi za kimataifa kuliko timu yoyote ile nchini.

Kwa nini Simba ilipoteza mechi yake ya pili kwenye Ligi ya Mabingwa? Mwandishi wa makala haya anaainisha jinsi mechi hiyo ilivyokuwa...

## HAIKUISOMA VEMA RAJA CASABLANCA

Ukiiangalia mechi hiyo, sidhani kama benchi la ufundi la Simba liliwaoma vema wapinzani wao. Badala yake ilicheza inavyocheza siku zote. Hawakuangalia ni wachezaji gani hatari ambao wanaweza kusambaza mipira kwao na kuwa hatari.

Nadhani ilifikiria kuwa timu za Waarabu huwa na tabia ya kuzuia sana wanapocheza ugenini. Lakini haikuwa hivyo kwa asilimia zote. Raja Casablanca iliikuwa inaisubiri wenzao washambulie, halafu kwa sababu walikuwa na uwezo wa kuzuia na kukaa na mpira wapandisha mashambulizi kwa haraka kwenda mbele na mpangilio maalum, ambayo yalikuwa ya hatari sana.

Kuna wakati baada ya kuona wamewakamata Simba, waliamua kutawanyika na kusakata kandanda bila kukaa nyuma, wakionyesha ufundi waliojaliwa nao miguuni.

## SIMBA SASA IMEZOELEKA

Wakati Simba inaonekana haikuisoma Raja Casablanca, uwezo wao kitimu, kimbinu na mchezaji mmoja mmoja, kinyume chake ni kwanza wapinzani wao walionekana kufahamu wanakwenda kucheza na timu ya aina gani.

Ukiwaangalia viungo na mabeki wa timu hiyo, walionekana kudili zaidi na mipira ya kupenyezwa kati. Ubora wa Simba siku zote haupo kwenye kupiga krosi na kufunga. Huwa wanapitia kati kufunga mabao yao. Mabeki wa viungo wa timu hiyo walionekana kucheza kwa maelekezo na kuzuia pasi zote mpenyezo.

Kama vile haitoshi, inaonekana waliwafahamu Clatous Chama na Saido Ntibazonkiza kuwa ndiyo wapishi wa timu hiyo, ndiyo maana hawakuwapa kabisa nafasi hata ya kukaa na mpira, au kuwaacha wafikiri.

Wanapogusa mpira tayari kuna mtu ambaye alikuwa anafanya kazi ya kumghasi ili asilete madhara. Ndiyo maana kwenye mechi ya juzi Chama na Saido ukiangalia kwa haraka haraka ni kama hawakuwa kwenye viwango vyao, la hasha.

Hawakuachiwa hata sekunde chake za kukokota mpira kwenye eneo la hatari na kufikiri cha kufanya. Hiyo peke yake iliinyima Simba kupata nafasi nyingi ambazo huwa inazitengeneza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Ukweli kwamba Simba ina wachezaji wengi ambao wamecheza misimu mitano Ligi ya Mabingwa, hivyo kusomeka ni rahisi sana na imeshazoeleka na kutengenezewa mpango mkakati wa kudhibitiwa.

## KUTOCHEZESHA MASTRAIKA WAWILI

Kwa sababu Simba ilihitaji zaidi ushindi, makocha walipaswa kuweka mastraika wawili ili kuweza kufanya mashambulizi mengi langoni mwa wapinzani wao.

Kuwapo kwa Bocco tu mbele, huku akiwa amebanwa na mabeki wawili warefu, hakukuwa na tija yoyote kwa wenyeji, badala yake walikuwa wakifanya mashambulizi kwa kubahatisha zaidi, tofauti na wapinzani wao ambao walishambulia kwa mpangilio na ya hatari.

Kuna wakati Shomari Kapombe alipokuwa anakwenda kupiga krosi, mbele kulikuwa na Bocco tu, halafu nyuma yake hakukuwa na mtu yeyote.

Katikati ya kipindi cha pili ambapo Jean Baleke na Mosses Phiri walipokuwa ndani ya uwanja, ulikuwa unaona sasa Simba yenye uhai na ndicho kipindi yalipigwa mashuti yenye kulenga lango, yote yakipigwa na Mzambia Phiri.

Nadhani huenda hali ingekuwa tofauti kama wangeanza, au Bocco angekuwa na msaidizi tangu mwanzo.

## RAJA CASABLACA ILICHEZA KIKUBWA

Kuna funzo ambalo inabidi timu za Tanzania ilipata kwenye mechi hiyo, kwani pamoja na kwamba ilionekana wachezaji wa Raja Casablanca wana uwezo mkubwa wa kuchezea mpira, lakini hawakuwa na mbwembwe nyingi.

Badala yake walikuwa wanacheza soka la moja kwa moja ili kupata ushindi tu na si vinginevyo. Soka la maelekezo na si la kufurahisha jukwaa.

Hawakufanya mashambulizi mengi sana langoni mwa Simba, lakini kila shambulizi lao lilikuwa la hatari mno. Mawinga wao hawakupiga krosi wanapofika kwenye mstari, walikuwa wanaangalia nani yupo eneo sahihi.

Zilikuwa ni krosi pasi. Wachezaji wao walikuwa wanagawanyika wanapoingia kwenye eneo la hatari. Wengine wanakuwa langoni na baadhi nyuma, mbali kidogo ya lango. Wale wanaokuwa nje kidogo ya lango ndiyo huwa hatari zaidi.

## VIWANGO VYA TIMU VIMEAMUA MECHI

Hata kama mechi ya juzi ingechezwa mpaka asubuhi ya jana, sidhani kama Simba ingeweza kurudisha mabao hayo. Labda kuongezwa. Ilionekana kabisa utofauti wa viwango vya wachezaji wa timu hizi mbili.

Wachezaji mmoja mmoja wa Raja Casablanca walikuwa na viwango vikubwa zaidi tofauti na Simba. Kwa bahati nzuri kwao, hata kiufundi na maelekezo kutoka kwa kocha wao walikuwa bora zaidi.

Mechi iliamuliwa zaidi na viwango vya wachezaji na ukubwa wa timu. Ukiiangalia Raja Casablanca ni timu yenye kiwango cha kuweza kufika hata fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu huu.

**JE, WAJUA?**



KIPIGO cha mabao 3-0 ilichokipata Simba katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi dhidi ya Raja Casablanca ni cha kwanza kwa klabu hiyo kupoteza mchezo wake uwanjani hapo katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.



## Askofu ataja dawa kukabiliana athari mabadiliko tabianchi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kulima kilimo kinachozingatia uhifadhi wa mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi.

Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Shinyanga, Johnson Chinyong'ole, alitoa rai hiyo juzi alipokuwa akizindua Kituo cha Kilimo kwa njia ya Mungu kilichoko eneo la Mtumba, kupitia mradi wa Care of Creation Tanzania.

Askofu Chinyong'ole, alisema kutokana na ongezeko la joto linalotokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ipo haja kwa Watanzania kuzingatia kilimo ambacho kitakuwa na faida katika utunzaji wa mazingira.

"Utunzaji wa mazingira umeelezwa hata katika vitabu vitakatifu kwani Mungu alipoumba ulimwengu alitengeneza bustani ambayo Adamu alikabidhiwa kuitunza, hivyo hatuna budi sisi wakulima kuhakikisha kuwa kilimo chetu kinazingatia ulinzi wa mazingira na uumbaji wa Mungu,"alisema.

Aidha, alisema kilimo cha asili kinafaida nyingi katika utunzaji wa mazingira pamoja na usalama wa chakula.

"Kilimo hai kinatupa mazao yenye ubora ambayo yamelimwa pasipo kutumia mbolea za kemikali hali ambayo itasaidia kulinda afya za walaji,"alisema.

Alisema kama kituo hicho kitatumika ipasavyo kitasaidia kuwajengea maarifa wananchi wengi ili kulima kilimo chenye tija kwa kupata mazao mengi pamoja na kulinda mazingira.

"Kilimo kwa njia ya Mungu ni kilimo ambacho lengo lake ni wakulima kulima lakini huku uumbaji wa Mungu ukiendelea kutunzwa ikiwa ni pamoja na upandaji wa miti,"alisisitiza.

Meneja wa Mradi huo, Alice Tlustos, alisema kuwa mradi huo umeonyesha faidi nyingi ambazo kama zitaendelezwa Tanzania inaweza kuwa kapu la chakula kwa Afrika na nje ya Afrika.

Alisema mradi huo ulianza Julai 2017 ambapo vibarua 800 walisaidia kuandaa eneo kwa kuchimba mitaro kwa ajili ya kukinga maji yatakayotumika kwa kilimo endelevu.

"Wakapanda miti na mimea mingine na kuanza kilimo kwa njia ya Mungu, Mheshimiwa mgeni rasmi hadi sasa Care of Creation Tanzania na wafanyakazi 32 walioajiriwa na mafundi pamoja na vibarua wamepanda miti zaidi ya 25,000 na kukusanya maji ya mvua lita milioni mbili,"alisema.

# Waandishi wamtunuku tuzo ya heshima Samia

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametunukiwa tuzo ya heshima na Klabu ya Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Dodoma (CPC), kutokana na dhamira yake ya kuhakikisha uhuru wa vyombo vya habari unaimarika na kushughulikia kwa vikwazo vinavyoikabili sekta ya habari nchini.

**Pia, tuzo ya mwandishi bora wa habari Mkoa wa Dodoma kwa mwaka 2022 alishinda Augusta Njoji kutoka Nipashe.**

Tuzo hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki kwenye hafla ya usiku wa CPC iliyoandaliwa kwa udhamini wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji(EWURA), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi ya Wazo Huru.

Mgeni rasmi wa hafla hiyo alikuwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo Mathew.

Akitoa maelezo ya tuzo hiyo iliyopokelewa kwa niaba na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule ambaye ni mlezi wa chama hicho, Mwenyekiti wa kamati ya utoaji tuzo, Nelly Mtema, alisema Rais Samia alipoingia madarakani aliagiza kufunguliwa kwa vyombo vya habari vilivyokuwa vimefungwa na kuanzishwa kwa mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Habari nchini ya mwaka 2016 iliyokuwa ikilalamikiwa na wadau kwenye baadhi ya vipengele.

"Pia katika uongozi wa Rais Samia amefanikisha kubadilishwa kwa viwango vya ada za usajili wa video za mtandaoni ambapo kwa sasa ni Sh. 500,000 badala ya Sh. milioni moja, hatua hii imewezesha waandishi wengi chipukizi kujiajiri kwa kufungua chaneli hizo," alisema.

Kuhusu uchumi wa vyombo vya habari na waandishi wa habari, Mtema alisema kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imeundwa kamati maalum ya kuchunguza hali ya kiuchumi kwa vyombo vya habari na waandishi wa habari ili kunusuru uchumi wa sekta hiyo.

Aidha, alisema tuzo ya kiongozi bora wa kitaifa kwa mwaka 2022, imetolewa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo kutokana na kuwa kiongozi anayezingatia muda katika utekelezaji wa majukumu yake hasa yanayohusisha waandishi wa habari.

Katika hafla hiyo, CPC ilitoa tuzo ya kutambua mchango wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwenye tasnia ya habari iliyopokelewa na Naibu Waziri Kundo huku Mkuu wa Mkoa Senyamule akipewa tuzo ya kutambua ushirikiano anaowapa waandishi wa habari wa Dodoma kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

Pia, tuzo ya mwandishi bora wa habari Mkoa wa Dodoma kwa mwaka 2022 alishinda Augusta Njoji kutoka Nipashe.

Pia tuzo ya ofisa habari bora ilikwenda kwa Nteghejwa Hosea kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, mwanachama bora wa CPC ilikwenda kwa Jackline Victor na tuzo ya mwandishi chipukizi ilitolewa kwa Rasul Kidindi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Naibu Waziri Kundo, alimshukuru Rais Samia kwa kuendelea kuboresha mazingira ya waandishi wa habari na kuweka misingi ya kisheria ili kupata taarifa.

Alisema: "Katika gharama ya usajili wa blogu Rais Samia aliagizwa zipitiwe upya na zikapitiwa na tutaendelea kufanya mapitio ili kufikia hatua ambayo kweli itasaidia wanahabari," alisema.



Meneja Msaidizi wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Dodoma, Syliver Rutagwelera, akizungumza na waandishi wa habari jijini humo, kuhusu mafanikio na majukumu ya mamlaka hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TRA yatoa elimu ya kodi kwa wafanyabiashara 4,499

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MAMLAKA ya Mapato nchini (TRA) mkoani Dodoma imesema kwa kipindi cha kuanzia Januari 2021 hadi Desemba 2022 wametoa elimu kwa walipakodi 4,499.

Imesema inatarajia kujipanga kuelekeza nguvu hiyo maeneo ya vijijini kutokana na kutokuwa na elimu hiyo.

Meneja Msaidizi TRA Dodoma ,Syliver Rutagwelera, aliyasema hayo jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo.

Rutagwelera alisema walipa kodi wa vijijini na pembezoni mwa miji hawana elimu kuhusu ulipaji kodi zinazotozwa na serikali.

Alisema kutokana na hali hiyo TRA Mkoa wa Dodoma wameanza kampeni ya kutoa elimu ya ulipaji kodi kwa maeneo hayo ili kuongeza walipa kodi wapya.

Alitaja miji midogo waliyotoa elimu mkoani Dodoma ni Mrijo, Soya, Chipogolo, Mtera, Mbande na Songambele, Mkoka, Tubugwe, Hombolo, Mvumi Misheni na Kibakwe.

Aidha, alisema kwa kipindi hicho wamesajili walipakodi wapya 12,076 na wengine 2,237 wanaotumia mashine za kielektroniki kwa mwaka 2022 pekee.

Alisema TRA wameendelea na juhudi za kusimamia matumizi ya mashine hizo kwa kutoa elimu na pia kutoa adhabu kwa wanaokiuka sheria.

Pia alisema TRA imekusanya mapato ya Sh.bilioni 82.6 kwa mwaka 2019/20 , mwaka 2020/2021 walikusanya Sh.bilioni 182.2 na mwaka 2021/2022 walikusanya Sh. bilioni 190.8.

Rutagwelera alisema kuanzia Februari 6 mwaka huu TRA imeanzisha utaratibu wa walipakodi wapya kujisajili kwa njia ya mtandao wakiwa popote pale bila kulazimika kufika ofisi zao.





# Kigogo ERB aona fursa masomo ya sayansi wanafunzi wa kike

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATOTO wa kike wametakiwa kuchangamkia masomo ya sayansi ili wajiunge na fani za kihandisi na kuongeza idadi ya kundi hilo kwenye shughuli za ujenzi wa miradi mbalimbali.

Wito hiyo umetolewa na Msajili wa Bodi ya Wahandisi nchini (ERB), Mhandisi Bernard Kavishe, mwishoni mwa wiki jijini Mbeya wakati wa kuwaapisha wahandisi wapya sita wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema kumekuwa na idadi ndogo ya wanawake wahandisi nchini tatizo ambalo linasababishwa na kundi hilo kuwa na msingi mbovu wa masomo ya sayansi ambayo yanatakiwa kwa mtu anayetaka kusomea fani hizo.

Alisema wanawake wachache waliopo kwenye fani hiyo huwa wanafanya vizuri wanapokabidhiwa miradi na hivyo akawataka Watanzania kulisaidia kundi hilo.

"Tutaongeza nguvu ya kuwahamasisha kuanzia shuleni ili wapende masomo haya na wajiunge na masomo ya sayansi ili wasomee fani za kihandisi, kwenye fani zetu hizi tuna idadi ndogo sana ya wanawake," alisema Mhandisi Kavishe.

Alisema katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini waliwaapisha wahandisi sita lakini wa kike walikuwa wawili pekee.

Hivyo, aliwataka wazazi na wadau mbalimbali kushirikiana na serikali kuhamasisha watoto wa kike kuyapenda masomo ya sayansi.

Akiwaapisha wahandisi hao, Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, Zawadi Laizer aliwataka wahandisi hao kwenda kufanya kazi kwa kuzingatia sheria.

Hivyo aliwataka kuzingatia kiapo walichoapa kwa maelezo kuwa wakikiuka watachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kushtakiwa.

Hakimu Laizer alisema moja ya mambo yatakayowafanya wachukuliwe hatua za kisheria ni pamoja na kutekeleza miradi chini ya kiwango na kuisababishia serikali hasara ama kushiriki kuhujumu miundombinu.

"Wakati mnaapa mlikuwa mnamtaja Mungu kwahiyo hakikisheni mnaheshimu viapo vyenu, nendeni mkafanye kazi kwa weledi huku mkiepuka rushwa kama ambavyo mmetamka," alisema Hakimu Laizer.

Aliwapongeza wanawake waliojitokeza kusomea fani hiyo ya uhandisi na kuwataka kwenda kufanya kazi vizuri ili wawaaminishe na wengine kwamba fani hizo siyo za wanaume pekee.

Baadhi ya wahandisi walioshuhudia viapo hivyo waliwashauri wahandisi chipukizi kuzingatia miiko ya taaluma hiyo wakati wa kutekeleza majukumu yao ili kuepuka kuichafua taaluma hiyo.

Mmoja wa wahandisi hao, Joseph Mkisi ambaye ni Mhandhiri Mstaafu wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), alisema fani hiyo ni miongoni mwa fani nyeti ambazo zinatakiwa kufanyika kwa weledi.

Alisema ipo miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na kundi hilo na kwamba endapo wahusika watakiuka miiko wanaweza wakasababisha matatizo kwa wananchi.

Alisema fani hiyo inahusu ujenzi na usimamizi wa miradi kama barabara, majengo, mabwawa na madaraja na kwamba endapo washiriki watatekeleza kwa kukiuka miiko ya fani hiyo wanaweza wakasababisha miradi hiyo kuharibika mapema na kusababisha madhara.

Nao baadhi ya wahandisi walioapishwa waliahidi kwenda kufanya kazi kwa weledi na kuisaidia serikali kupunguza gharama za kuajiri wahandisi kutoka nje ya nchi kwenye utekelezaji wa miradi.



Wasamaria wema wakimsaidia dereva bodaboda kusukuma pikipiki yake baada ya kupata hitilafu kwenye moja ya milima iliyoko Kata ya Ileya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Magari ya abiria, mizigo yakaguliwa kudhibiti ongezeko ajali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya, limezindua rasmi wiki ya nenda kwa usalama kwa kuanzisha ukaguzi maalumu wa magari ya abiria na mizigo ili kukabiliana na tatizo la ajali ambalo limekuwa likiukumba mkoa huo mara kwa mara.

Uzinduzi huo ulifanyika katika eneo la mteremko wa Shamwengo nje kidogo ya Jiji la Mbeya mahali ambapo ajali zimekuwa zikitokea mara kwa mara kutokana na mteremko mkali pamoja na ufinyu wa barabara katika eneo hilo.

Akizindua wiki hiyo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi Benjamin Kuzaga, aliwataka wananchi na wadau mbalimbali wa usafiri na usafirishaji kushiriki kwenye kuzuia ajali za barabarani ambazo zinaweza zikazuilika.

Kamanda Kuzaga aliwataka madereva wa vyombo vya usafiri kuzingatia sheria za usalama barabarani wakati wa kuendesha vyombo hivyo ili kuepuka kusababisha ajali.

Alisema mara nyingi ajali ambazo zimekuwa zikitokea, zimekuwa zikisababisha vifo, majeraha na ulemavu wa kudumu kwa baadhi ya wananchi wasiokuwa na hatia pamoja na uharibifu wa mali.

"Tunapoizindua siku hii naomba wote tushirikiane, madereva zingatieni sheria za usalama barabarani, epukeni kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari," alisema Kamanda Kuzaga.

Aliwataka wakaguzi wa jeshi hilo kuhakikisha wanazingatia weledi wakati wa kukagua magari hayo na kuhakikisha magari yote yanayobainika kuwa na hitilafu yanasitishiwa safari mpaka yatengenezwe.

# CCM kuwaadhibu wanachama wanaowatukana viongozi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya kimesema kitawachukulia hatua kwa mujibu wa katiba ya chama hicho wanachama wake wanaowatukana na kuwakosoa viongozi wa chama na wa serikali bila staha.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu (NEC) ya chama hicho, Ndele Mwaselela, alitoa onyo hilo juzi wilayani Chunya alipokuwa anazungumza na viongozi wa chama hicho kutoka katika kata zote za wilaya hiyo.

Alisema chama hicho kina utaratibu wa kuzungumza mambo yanayohusu utendaji wa viongozi wake kupitia vikao vya kikatiba na kikanuni ambavyo kazi yake ni kukosoana na kuelekezana kuhusu mambo mbalimbali.

Alisema mtu yeyote ambaye anawakosoa viongozi wa chama hadharani anakuwa anakiuka miiko ya chama hicho na hivyo watawachukulia hatua ili iwe fundisho kwa wengine.

"Tukikukuta wewe umevaa sare za CCM halafu unawasema viongozi wa chama hadharani tutanyooka na wewe maana hapo utakuwa unakisema ni chama chenyewe jambo ambalo ni kinyume na katiba yetu," alisema Mwaselela.

Alisema serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo inawagusa moja kwa moja wananchi na hivyo kazi inayotakiwa kufanywa na viongozi wa chama ni kuhakikisha wanaitangaza miradi hiyo kwa wananchi.

Alisema wataendelea kuhakikisha wanaendelea kuisaidia serikali kusimamia miradi kwa kuhakikisha inatekelezwa kwa weledi na ufanisi mkubwa zaidi.

Hivyo, aliwataka viongozi wa chama hicho kuendelea kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya chama hiyo kwa kuhakikisha wanashiriki kukagua miradi inayotekeleza.

Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka alisema katika Wilaya ya Chunya, Serikali imeboresha huduma mbalimbali za kijamii ikiwamo huduma za afya, elimu, maji na usambazaji wa huduma ya umeme hasa maeneo ya vijijini.

Alisema serikali imejenga vituo vya afya na zahanati kwenye vijiji na kata mbalimbali ambazo awali wananchi walikuwa wanalazimika kwenda kutibiwa katika Hospitali ya Wilaya.

Alisema katika baadhi ya maeneo ambayo huduma hiyo bado haijafika, serikali inaendelea na michakato mbalimbali ya kuhakikisha huduma hizo zinawafikia wananchi hasa huduma ya umeme kupitia Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini (REA).

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, Bashiru Madodi, alisema baada ya uchaguzi wa MNEC kuahirishwa awali ilitokea hali ya sintofahamu miongoni mwa baadhi ya wanachama wa chama hicho.

Alisema kikatiba Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa anachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa lakini kwa sasa hivi haikufanyika hivyo na badala yake alichaguliwa na Halmashauri Kuu ya Mkoa kutokana na hitilafu iliyokuwa imetokea mwanzo.

Alisema kwa mujibu wa Katiba ya chama hicho, Halmashauri Kuu ya Mkoa ina wajibu wa kujaza nafasi yoyote ambayo inakuwa iko wazi na kwamba ndicho kilichokuwa kimefanyika kwa nafasi ya MNEC baada ya uchaguzi mkuu kumalizika mwishoni mwa mwezi Desemba mwaka jana.



# ZPC yajinasibu kumaliza tatizo mrundikano mizigo bandarini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Bandari Zanzibar (ZPC) limesema baada ya siku saba linatarajia kumaliza tatizo la mrundikano wa bidhaa baada ya kuanzisha mifumo mipya ya uondoshaji wa mizigo katika bandari hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Nahati Mohamed Mahfoudh, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Bandarini Malindi Mjini Zanzibar.

Alisema uamuzi huo umefikiwa baada ya shirika hilo kukaa na wadau kuamua bidhaa zote zinazofanana zitashushwa nje ili kupunguza mrundikano wa makontena yaliyokuwa hayana kazi kwenye bandari hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema hivi sasa shirika limejipanga kufanya kazi saa 24 kwa lengo la kuondoa msongamano wa makontena ambayo ni kikwazo kwa baadhi ya shughuli za ndani ya bandari hiyo.

"Hivi sasa bandari imekuja na mbinu mbadala kwa kuweka kifaa maalum cha kushushia makontena ambacho kitarahisisha upakuaji wa makontena kutolewa ndani ya meli na kuokoa muda kwa lengo la kupatikana unafuu wa kuingia meli zingine kwenye ukuta wa kushushia mzigo,"alisema.

Alieleza kuwa, hali hiyo imekuja kutokana na kuchelewa kushushwa bidhaa hasa katika kipindi kijacho cha mfungo wa Ramadhan na kusababisha bidhaa nyingi kuchelewa ikiwamo mchele, unga, sukari, tende na bidhaa zingine.

Alisema endapo makontena yatatolewa nje ya bandari itawarahisishia watu wanaofika bandarini kufuata mizigo yao na kupunguza msongamano usiokuwa na tija.

Aidha alisema kwa kawaida kontena linapofika bandarini baada ya siku saba huwa linaanza kulipiwa ushuru na iwapo kontena hilo mmiliki atashindwa kulitoa mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) litalitaifisha au kupigwa mnada.

Alisema kuwapo kwa mfumo wa TEHAMA utarahisisha kujua meli inayoingia ina makontena mangapi lakini hata yaliyokuwapo bandarini hapo kujulikana idadi yake.

Hata hivyo alisema wadau na wafanyabiashara watashirikishwa katika kutoa maoni yao juu ya uingizaji wa mizigo na utoaji, hususani katika kipindi cha kuelekea mwezi wa Ramadhan.

Naibu Mkurugenzi wa shirika hilo, Akif Khamis, alisema kabla ya kufikia hatua za kushusha mizigo iliyofanana walikaa na kutafakari na kufikia makubaliano hayo.

Alisema tayari wameshazungumza na TRA na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), katika suala zima la kufanyiwa uhafifu wa kodi kwa wafanyabiashara wanapoingiza mizigo.

# SMZ kuwapa walimu mbinu za kufundisha ili kuongeza ufaulu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itawapatia mafunzo walimu mbinu za ufundishaji ili waongeze ujuzi, kuongeza ufaulu kwa wanafunzi katika mitihani yao ya taifa.

Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafuzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdallah Gulam, aliyasema hayo juzi Mjini Zanzibar katika hafla ya ugawaji wa vyeti kwa walimu wa sayansi na hisabati waliopatiwa mafunzo ya mbinu bora za ufundishaji kupitia mradi wa kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari.

Alisema ili ufaulu wa wanafunzi uongezeke lazima kuwe na msingi mizuri ya mazingira ya utoaji wa elimu, kujenga miundombinu ya kisasa, kufanya ukarabati wa madarasa chakavu, kujenga shule mpya pamoja na kuboresha maslahi ya walimu.

Alisema serikali inafanya jitihada hizo za kuboresha miundombinu ya upatikanaji wa elimu ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi katika mitihani yao ya taifa.

**Rais Dk. Mwinyi anataka kuona matokeo ya ufaulu unaongezeka kwenye masomo ya sayansi na kuwataka walimu kufanya kila linalowezekana ili matokeo hayo yaongezeke mara dufu.**

Gulam alisema mafunzo hayo ni muhimu, hivyo aliwasisitiza walimu kuyatumia mafunzo hayo kama ilivyokusudiwa.

"Kuna mtindo ambao siyo mzuri kwa baadhi ya walimu kupatiwa mafunzo lakini baada ya muda mfupi mwalimu hao hupeleka barua wizarani ya uamisho bila ya kuyafanyia kazi mafunzo aliyopatiwa," alisema.

Aidha, alisema jambo hilo halipendezi kwasababu serikali inamwandaa mwalimu huyo kwa kutumia fedha ili ayafanyie kazi lakini baada ya muda mfupi mwalimu huyo anaenda katika taasisi nyingine.

Alisema haikatazwi mtu kwenda katika taasisi nyingine lakini wizara itahakikisha kuwa inawabana walimu hao kwa kutoruhusu uhamisho usiokuwa na maslahi kwa taifa na elimu.

"Tushawekeza, tushakujenga halafu kesho unakwenda sehemu ambayo huitumii ile taaluma yako ambayo tumekutengea baada ya muda unatupa mzigo sisi kuendelea kuajiri tena jambo hilo hatutakubali," alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Abdallah Said, alisema mradi huo umegharimu shilingi bilioni 23.

Alisema Rais Dk. Mwinyi anataka kuona matokeo ya ufaulu unaongezeka kwenye masomo ya sayansi na kuwataka walimu kufanya kila linalowezekana ili matokeo hayo yaongezeke mara dufu.

Alisema mafunzo hayo tayari yameanza kuleta matokeo chanya, kwamba kuna ufaulu wa daraja la kwanza zaidi ya 700 kwa matokeo ya kidato cha nne mwaka huu jambo ambalo halijawahi kutokea Zanzibar.

Meneja Mwandamizi wa Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari Zanzibar, John Masenza, alisema mradi huo ni wa miaka mitano unaofadhiliwa na KOICA na kutekelezwa na Taasisi ya Good Neighbour.

Alisema mafunzo hayo yaliojumuisha walimu 1,357 lengo kuwajengea uwezo walimu ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji wao.



Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid (kulia), akipokea vitabu kwa Balozi mdogo wa China anayefanyia shughuli zake Zanzibar, Zhang Zhisheng, kwa ajili ya maktaba kwenye ofisi za Baraza la Wawakilishi, hafla ya makabidhiano ilifanyika Chukwani Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# UNESCO, TAMWA zaingia makubaliano kuwajengea uwezo wanahabari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar) zimesaini mkataba wa mradi wa kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuandika habari za kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Mradi huo wa miezi mitatu wenye thamani ya Dola za Marekani 17,000, umesainiwa kati ya Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa Ali na Mwakilishi Mkazi wa UNESCO Tanzania, Michael Toto.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Mzuri alisema mradi huo utaongeza nguvu ya mapambano dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto ambayo ni moja ya mikakati inayotekelezwa na serikali.

Alisema ni mara ya kwanza kwa TAMWA na UNESCO kushirikiana katika mapambano hayo na kuahidi kutekeleza mradi huo kwa kiwango ili kukidhi matarajio.

Alisema anamatumaini makubwa kwamba mradi huo utafanya vizuri na kuleta tija kwa maslahi ya taifa.

Mwakilishi Mkaazi wa UNESCO Tanzania, Michel Toto, alisema mradi huo utalenga kuwajengea uwezo wanahabari katika kuondoa mila potovu kuhusu masuala ya kijinsia visiwani Zanzibar.

Kadhalika, alipongeza mchango wa wanahabari na TAMWA kwa kujikita kuandika habari za udhalilishaji na kuahidi kwamba UNESCO itaendelea kushirikiana na TAMWA katika kukabiliana na matukio ya udhalilishaji ikiwamo kupunguza mimba za umri mdogo.

# Kikongwe wa miaka 80, mwenzake jela miaka 20

**Na Grace Gurisha**

BABU wa miaka 80, Vincent Mtekela na Christopher Kipilili (56) wamehukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni 80 au kutumikia kifungo cha miaka 20 gerezani baada ya kupatikana na hatia ya kukutwa na ngozi ya chui.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi Mwandamizi Evodia Kyaruzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam baada ya kupitia ushahidi na utetezi uliotolewa na pande zote mbili na kuwaona washtakiwa wote wana hatia.

Hakimu Kyaruzi alisema aliridhishwa na ushahidi uliotolewa na mashahidi watano wa upande wa mashtaka pamoja na vielelezo ambavyo vilithibitisha pasipo kuacha shaka.

"Mahakama inawahukumu kila mmoja kulipa faini ya Sh. milioni 80 ama kutumikia kifungo cha miaka 20 gerezani," alisema Hakimu Kyaruzi.

Hakimu huyo alisema rufani kwa washtakiwa iko wazi kama hawajaridhika na adhabu hiyo.

Kabla ya kuwasomea washtakiwa adhabu hiyo, hakimu aliuliza upande wa mashtaka kama ulikuwa na lolote la kusema kuhusu washtakiwa.

Wakili wa Serikali, Monica Ndakidemi aliomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa washtakiwa ili iwe fundisho kwao na kwa watu wengine.

"Hatuna kumbukumbu za makosa ya nyuma dhidi ya washtakiwa, lakini tunaomba mahakama itoe adhabu kali kwani kosa hilo ni hatari na linaaathari maliasili ya nchi yetu," alidai Wakili Nkakidemi.

Katika utetezi wao, mshtakiwa Mtekela aliiomba mahakama imwonee huruma kwa kuwa ni mzee, hana uwezo wa kuona vizuri na mwili wake umeshachoka.

Mshtakiwa Kipilili aliiomba mahakama impunguzie adhabu na kumwonea huruma kwani ana familia inamtegemea na pia ni kosa lake la kwanza.

Katika kesi hiyo, inadaiwa kuwa Mei 9, 2018, huko Mburahati Kisiwani, Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam, washtakiwa walikutwa na nyara za serikali ambazo ni ngozi moja ya chui yenye thamani ya Sh. 8,050,000, mali ya serikali bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.




Katibu Tawala Wilaya ya Serengeti, Qamara Qamara (wa pili kushoto), akipokea vifaa vya ofisi kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Serengeti kutoka kwa Meneja wa Benki ya Azania tawi la Lamadi, Muhidin Mjuvi (kulia), mwishoni mwa wiki. Vifaa hivyo vimetolewa kwa Shule ya Msingi Kenyamonta iliyoko wilayani humo mkoani Mara. Wengine ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ayub Makuruma (kushoto) na viongozi mbalimbali wa shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT-Wazalendo kufanya mikutano 117 Lindi

**Na Said Hamdani, LINDI**

CHAMA cha ACT-Wazalendo mkoani Lindi kimejipanga kufanya mikutano ya hadhara 117 kwa ajili ya kunadi sera kwa wananchi.

Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo mkoani Lindi, Rashidi Mchinjita, aliyasema hayo jana wakati akihutubia wakazi wa Manispaa ya Lindi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Uwanja wa Sera mjini hapo.

Huo ni mkutano wa kwanza kufanywa na Chama cha ACT-Wazalendo mkoa wa Lindi tangu Rais Samia Suluu Hassan atoe rukhsa ya mikutano ya hadhara.

Mwenyekiti Mchinjita alisema kuzuiliwa kwa mikutano ya kisiasa kuliwanyima Watanzania nafasi ya kukaa pamoja na kueleza kero mbalimbali kwa viongozi wa vyama vya upinzani.

Mkurugenzi wa Vijana wa chama hicho mkoani Lindi, Deo Chaurembo, aliwashauri wanachama kujiunga na mfumo wa kadi kiganjani kwa kuwa una faida nyingi ikiwamo kupatiwa mikopo kupitia simu zao za mikononi bila masharti ya riba.

# Wanafunzi 2,344 hawajaripoti kidato cha kwanza Shinyanga

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

UONGOZI wa Mkoa wa Shinyanga umetoa wiki moja kwa wakuu wa wilaya na maofisa elimu kuhakikisha wanafunzi 2,344 ambao hawajajiunga na kidato cha kwanza wanaripoti.

Pia umeliagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kukamilisha upelelezi dhidi ya watuhumiwa wanaodaiwa kuwapa ujauzito wanafunzi, ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi yao.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yahaya Nawanda, aliagiza hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

Dk. Nawanda ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, alisema hajaridhishwa na mwenendo wa wanafunzi kuripoti shuleni mwaka huu, unaoonyesha wanafunzi 2,344 waliochaguliwa, hawajajiunga na masomo.

"Wakuu wa wilaya, maofisa elimu na watendaji wote wa serikali ninatoa wiki moja tu hadi kufika siku ya Jumatano (keshokutwa), nipewe taarifa kuwa wanafunzi 2,344 ambao hawajaripoti shuleni kuanza kidato cha kwanza, wawe darasani hata kama hawana sare za shule," aliagiza.

"Kama mnaona itakuwa ngumu, niambieni ili niingie mwenyewe mitaani kuwasaka hawa wanafunzi, ila ninaamini mtaweza lakini kama ikishindikana ninaingia mwenyewe, tunataka wanafunzi wote wapate elimu na kutimiza ndoto zao kama adhima ya Rais Samia Suluhu Hassan inavyotaka, ndiyo maana amekuwa akitoa fedha nyingi kujenga miundombinu ya elimu," alisema.

Kiongozi huyo aliliagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha linakamilisha upelelezi haraka wa kesi za mimba za wanafunzi, ili watuhumiwa wafikishwe mahakamani na kuchukuliwa hatua kali za kisheria na kuwa fundisho kwa watu wengine kuacha kufanya mapenzi na wanafunzi.

Awali Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, Dafroza Ndalichako, alitaja takwimu za wanafunzi waliopata ujauzito na kuacha masomo mwaka jana kuwa ni 147 kwa shule za msingi (mimba 28) na sekondari 119. Alifafanua kati ya wanafunzi 28 wa shule za msingi ambao walipewa ujauzito, kesi zilizoko mahakamani ni mbili na 26 ziko katika upelelezi.

Alisema kuna kesi 119 mimba kwa wanafunzi wa sekondari, 21 pekee zilipelekwa mahakamani, tatu zilitolewa hukumu, 22 zinaendelea kusikilizwa na kesi 38 upelelezi wake haujakamilika.

# Vita Ukraine, Biden kutoa neno Jumanne

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Joe Biden, anatarajiwa kutoa hotuba kesho nchini Poland katika maadhimisho ya mwaka mmoja wa uvamizi wa Russia nchini Ukraine na kwamba ataelezea nia ya taifa lake kuunga mkono ulinzi wa Ukraine.

Hayo yamebainishwa jana na Msemaji wa Baraza la Usalama wa Taifa wa Marekani, John Kirby, alisema wakati mashambulizi ya Russia yakiendelea nchini Ukraine, Biden ataadhimisha mwaka mmoja wa vita hivyo kwa hotuba katika nchi jirani ya Poland.

White House ilisema hakuna mipango kwa Biden kuitembelea Ukraine wala kukutana na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskyy wakati wa ziara yake, lakini wachambuzi wanasema kuna dalili wawili hao wanaweza kukutana Poland.

Viongozi hao wawili walikutana mwishoni mwa Desemba 2022 wakati Zelenskyy alipofanya ziara ya kushtukiza Washington DC.

Aidha, wadadisi wanasema Ukraine inaugeuza mzozo huo kuwa ni vita vya kushtukiza katika juhudi ya kuzima azma ya wa Ukraine na kuuchosha ustahimilivu wa Magharibi.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa Ukraine imekuwa na fursa nzuri ya kupata silaha za hali ya juu kutoka Magharibi, lakini Russia inanufaika kutokana na ukubwa wa uchumi wake, wafanyakazi na uwezo wa kiulinzi.

***VOA***



Wanajeshi wa Nigeria wakiwa wameshika bendera ya Boko Haram baada ya kuukomboa mji wa Damasak. **PICHA: VOA**

# Mwanadiplomasia Israel afukuzwa mkutano AU

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

KUMETOKEA sintofahamu ya kidiplomasia katika ufunguzi wa mkutano wa 36 wa Umoja wa Afrika (AU) mjini Addis Ababa nchini Ethiopia baada ya mwanadiplomasia wa Israel kufukuzwa kwenye sherehe za ufunguzi, kwa madai kwamba hakualikwa.

Video ya tukio hilo ilisambaa jana kwenye mitandao ya kijamii, ikionyesha maofisa wa usalama wa AU wakimsindikiza mwanadiplomasia huyo kutoka Israel ambaye ni Naibu Mkurugenzi wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Israel kwa Afrika, Sharon Bar-li, kutoka nje ya ukumbi wa mkutano.

Israel inaeleza kwamba kitendo hicho ni kibaya, huku msemaji wa mwenyekiti wa Kamisheni ya AU Ebba Kalondo, akieleza kuwa mwanadiplomasia huyo aliombwa kuondoka katika eneo hilo kwasababu balozi wa Israel katika Umoja wa Afrika, Aleli Admasu, ndiye aliyepokea mwaliko wa kibinafsi.

"Inasikitisha kwamba mhusika alitumia vibaya nafasi hiyo," alisema.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Israel ilisema Bar-li alipata kibali kwa njia nzuri na inayostahili kama mwangalizi, na inashutumu AU kuwa mateka wa idadi ndogo ya mataifa yenye msimamo mkali kama Algeria na Afrika Kusini.

Inaelezwa kuwa nyuma ya tukio hilo, kuna suala la hadhi ya Israel, ambalo halijatatuliwa, na kwamba mwaka jana, ilizuka mijadala baada ya Moussa Faki kutoa hadhi ya taifa hilo kuwa mwangalizi. Ikidaiwa kuwa tume iliundwa kuchunguza suala hilo nyeti lakini haijawahi kukutana.

Msemaji wa Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, Vincent Magwenya, aliliambia shirika la habari la AFP kwamba Israel inapaswa kuthibitisha shutuma zake.

Hata hivyo, kesi hiyo inaonekana vibaya kwa serikali ya Israel katika uhusiano wake na Afrika.

Inatajwa kuwa kwa Israel tukio hilo ni la aibu wakati ambao Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu, amejizatiti kuimarisha uhusiano na bara la Afrika kuwa mojawapo ya malengo makuu ya sera za kigeni za nchi yake.

Suala la hadhi ya waangalizi wa ujumbe wa Israel ndio chanzo cha mfarakano mkubwa ndani ya AU. Na kwamba katika mkutano wa kilele wa mwaka jana, mjadala kuhusu suala hilo ulisitishwa ili kuepusha kura iliyoonekana kuwa na matatizo.

Mara kadhaa, Mamlaka ya Ndani ya Palestina imewataka viongozi wa Kiafrika kuondoa kibali cha Israel kwa jumuiya hiyo ya bara, ikikashifu utawala wake unaoelezwa kuwa ubaguzi wa rangi.

Vile vile inabainishwa kuwa juhudi zinaendelea kuruhusu ujumbe wa Israel kushiriki kama mwangalizi katika mijadala hiyo.

***RFI***

## MNJTF yaikabidhi Cameroon watoto waliotekwa na Boko Haram

**YAOUNDE, Cameroon**

KIKOSI Kazi cha Pamoja cha Kanda cha Tume ya Ziwa Chad (MNJTF) kimesema kimekabidhi watoto watano kwa maofisa wa Cameroon baada ya kuokolewa na wanajeshi wa Chad na kwamba mamlaka inafanya kazi ya kuwatafuta wazazi wa watoto hao.

Aidha, inabainishwa kuwa watoto kadhaa waliokolewa mwaka jana katika operesheni dhidi ya kundi la wanamgambo wa kiislamu.

Kikosi kazi hicho kilisema wanajeshi wa Chad waliwagundua vijana watano katika eneo tete la Ziwa Chad, wakionekana wachafu, wenye njaa na wagonjwa.

Kamanda wa kikosi hicho, Meja Jenerali Abdul Kalifa Ibrahim kutoka Nigeria, alisema vijana hao walikaa kwa miezi kadhaa katika utumwa chini ya Boko Haram.

"Ilikuwa bahati mbaya walitekwa na Boko Haram, lakini waliweza kukimbia," alisema.

"Wanajeshi wa Chad waligundua kuwa ni watoto wa Cameroon, tutafanya operesheni zaidi, matumaini yetu ni kwa Boko Haram kujitokeza na kusema hii imetosha," alisema.

***VOA***

## Korea Kaskazini yarusha kombora kuthibitisha uwezo wake

**PYONGYANG, Korea Kaskazini**

VYOMBO vya habari vya serikali ya Korea Kaskazini vimesema nchi hiyo imerusha kombora la masafa marefu (ICBM) ili kuthibitisha kutegemewa kwa silaha hiyo katika kukabiliana na maadui.

Jaribio hilo lilitekelezwa jana na Kim Yo-jong, Dada wa Rais wa Korea Kaskazini Kim Jong-un, ambaye alisema vitendo vyovyote vya uhasama vitakabiliwa na jibu kali na kubwa.

Korea Kaskazini, ilisema jaribio hilo lilionyesha kuwa lina uwezo wa kukabiliana na vikosi vya uadui kama Marekani na Korea Kusini, na kwamba kombora hilo liliruka zaidi ya kilomita 900 kwa dakika 67 na kutua katika bahari ya Japan.

Inaelezwa kuwa hatua hiyo inakuja kabla ya mazoezi ya pamoja kati ya Marekani na Korea Kusini mwezi ujao, ambayo yaliandaliwa kukabiliana na vitisho vya nyuklia vinavyoongezeka vya Korea Kaskazini.

Mamlaka ya Korea Kaskazini, ilitishia kulipiza kisasi kwa nguvu isiyo na kifani kwa mazoezi yoyote kama hayo, ikisisitiza kuwa yanafanywa ili kujiandaa kuivamia Korea Kaskazini.

Pia dada wa Rais wa taifa hilo, Kim Yo-Jong, aliitaka Marekani kukomesha kile alichokiita vitisho dhidi ya serikali yake.

***BBC***

HABARI MICHEZO

# SIMBA QUEENS KILELENI MZUNGUKO WA KWANZA LIGI KUU UKIMALIZIKA

**Na Adam Fungamwango**

MZUNGUKO wa kwanza wa Ligi Kuu ya Wanawake umemalizika huku Mabingwa wa Soka Tanzania, Simba Queens, wakiwa kileleni mwa msimamo.

Mechi ya mwisho ya mzunguko huo ilikuwa juzi wakati Baobab ilipotoka suluhu dhidi ya Alliance Girls kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Baada ya mechi hiyo kumalizika, Simba Queens sasa iko kileleni ikiwa na pointi 22 kwa michezo tisa ambayo imecheza, ikishinda mechi saba, sare moja, ikipoteza moja, ikipachika mabao 29 nyavuni na kuwa timu inayoongoza kwa kuwa na mabao mengi mpaka sasa.

Haikuwa rahisi kwa timu hiyo kufika hapo, kwani ilibidi isubiri hadi raundi ya sita ndipo ilipofanikiwa, huku raundi zote hizo zilikuwa zikiongozwa kwa maafande wa JKT Queens ambayo msimu huu imeonekana inauhitaji ubingwa kwa udi na uvumba.

Ni timu ambayo inaonekana kuwa mshindani mkubwa wa Simba Queens kwenye kulisaka taji hilo.

JKT Queens kwa sasa imeshushwa hadi nafasi ya pili, lakini imeendelea kung'ang'ania hapo hapo hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, ikiachwa pointi moja tu na Simba Queens.

Ina pointi 21 ikicheza mechi tisa, kushinda sita, sare tatu na ndiyo timu pekee ambayo haijapoteza mechi yoyote kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, ikifunga mabao 23.

Timu ya Fountain Gate Princess, imemaliza mzunguko huo ikiwa kwenye nafasi ya tatu ikijikusanyia pointi 20, huku Yanga Princess ikiwa kwenye nafasi ya nne na pointi hizo hizo 20.

Timu hizo zinafanana kwa mechi zilizocheza, zote zilishinda mechi sita, sare mbili na kupoteza moja kila moja, zikifunga mabao 21. Hata hivyo, Fountain Gate Princess imefunga mabao manne ambayo ni machache dhidi ya Yanga ambayo imeruhusu mabao matano na kuifanya kuwa chini yake.

Nafasi ya tano inashikiliwa na Alliance Girls ikiwa na pointi 15 na timu inayoshika mkia ni Mkwawa Queens yenye pointi moja mpaka sasa.

Mzunguko wa pili wa Ligi Kuu unatarajiwa kuanza tena Aprili 18, mwaka huu, Baobab itakapocheza dhidi ya Fountain Gate Princess Uwanja wa Jamahuri Dodoma, The Tigers Queens dhidi ya JKT Queens, Uwanja wa Black Rhino, Karatu, Arusha na Yanga Princess dhidi ya Ceasiaa Queens, katika dimba la Uhuru, Dar es Salaam.

MILIKI...



Beki wa Simba, Shomari Kapombe (kulia), akimiliki mpira dhidi ya winga wa Raja Casablaca ya Morocco, Yousri Bouzok, kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na wenyeji kuchezea kichapo cha mabao 3-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Dodoma Jiji yaihofia Ihefu

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Dodoma Jiji FC, Kassim Liogope, amesema kuwa mechi yao dhidi ya Ihefu inayotarajiwa kuchezwa Ijumaa ijayo, itakuwa ni ngumu kutokana na timu hiyo kuonja joto la kukaa mkiani, hivyo haitotaka kurejea tena ilikokuwa.

Akizungumzia kuhusu maandalizi ya mechi hiyo, alisema wamejipanga vema kukabiliana na timu hiyo ambayo kwa sasa imekuwa tishio kutokana na kufanya usajili mzuri wa wachezaji wakubwa na wa kimataifa.

"Ihefu na sisi ni timu ambazo hatujaachana sana, ni ngumu sana kwenda kucheza na timu ambayo ilikaa chini kwa muda mrefu, haitokubali kutoka kule ilikotoka.

Hata sisi tulikaa nao kule chini, lakini wenzetu kwa sasa wapo juu kidogo, wamefanya usajili mzuri, nadhani mechi itakuwa nzuri sana," alisema Liogope.

Dodoma Jiji inakwenda kucheza mechi hiyo ikiwa kwenye uwanja wa nyumbani, Jamhuri Dodoma, ikiwa na machungu ya kufungwa mabao 2-1 Jumamosi iliyopita dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro.

Timu hiyo inashika nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 24 kwa mechi 23 ambazo imecheza, hivyo kuwa moja kati ya timu zinazohitaji zaidi ushindi ili kujiondoa kwenye eneo hatari ambalo linaweza kusababisha kushuka daraja au kwenda kucheza mechi za mchujo ili kubaki au kushuka.

Timu zitakazomaliza nafasi ya 16 na 15 zitashuka daraja moja kwa moja na zitakazoshika nafasi ya 14 na 13 ligi itakapomalizika, zitakwenda kucheza mechi za mchujo na timu zitakazoshika nafasi za tatu na nne kwenye Ligi ya Championship, ili kupata timu zitakazobaki Ligi Kuu au kuteremka.

# Pawassa anasa 10 mashindano ya majeshi

**Na Hadija Mngwai**

KUELEKEA maandalizi ya mchezo wao dhidi ya Morocco Machi, mwaka huu, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Soka la Ufukweni, Boniface Pawassa, amefunguka kuwa amefanikiwa kunasa nyota 10 katika mashindano ya Majeshi yaliyomalizika hivi karibuni mkoani Mtwara.

Benchi la ufundi la Timu ya Taifa ya Soka la Ufukweni lilikuwa lilikita kambi mkoani Mtwara hivi karibuni kusaka vipaji kwa ajili ya timu hiyo, hivyo kutoka na wapya 10. Akizungumza na Nipashe jana, Pawassa alisema kambi yao waliyoweka mkoani Mtwara imefanikiwa kwa asilimia 75 baada ya kupata nyota 10 watakaoingia kambi kujiwinda na mchezo huo dhidi ya Morocco.

"Tulikuwa Mtwara kwenye mashindano ya Majeshi ambapo benchi zima la ufundi tulikuwa pale kuweza kung'amua wachezaji kutokana na mahitaji yetu na tumeweza kufanikiwa kwa asilimia 75.

"Tumepata jumla ya wachezaji 10 kwenye mashindano haya ya Majeshi, wachezaji hawa tutawatangaza na tutaingia kambini mwanzoni mwa Machi," alisema Pawassa.

"Tuna mechi dhidi ya Morocco ambapo tutacheza kati ya tarehe 25 na 26 Machi, tunasubiria kuanza kambi yetu mapema baada ya mashindano ya Cecafa kumalizika ndio tutaingia kambini hii ndio ratiba yetu ya michuano ya Beach Soccer," alisema Pawassa.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RUDIGER ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kumsajili beki wa Real Madrid na Ujerumani, Antonio Rudiger, mwenye umri wa miaka 29, katika dirisha la usajili la majira ya joto. ***(Fijaches)***

### DE GEA KUBAKIZWA

MANCHESTER United iko tayari kuongeza mshahara wa David de Gea hadi kufikia pauni 250,000 kwa wiki ili kumbakisha kipa huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 32, pale Old Trafford, lakini klabu hiyo tayari inamtazama mlinda mlango wa Leeds United, Illan Meslier mwenye umri wa miaka 22, kama mbadala wake wa muda mrefu. ***(Sun)***

### RATCLIFFE OFA NDOGO

OFA ya bilionea, Sir Jim Ratcliffe ya kutaka kuinunua Manchester United ni pauni bilioni moja chini ya pauni bilioni tano iliyotolewa na Sheikh Jassim Bin Hamad Al Thani. ***(Foot Mercato)***

### WEST HAM YATAKA NYOTA

KLABU ya West Ham inaweza kutuma ofa ya kumnunua kiungo wa kati wa Manchester United na Scotland mwenye umri wa miaka 26, Scott McTominay. Pia inawataka Harry Maguire mwenye miaka 29, kiungo wa kati wa Uholanzi Donny van de Beek mwenye miaka 25 na mshambuliaji wa Ufaransa, Anthony Martial mwenye miaka 27. ***(CaughtOffside)***

### SAVIC ATAJWA WEST HAM

West Ham imemweka kiungo wa kati wa Lazio na Serbia, Sergej Milinkovic-Savic, mwenye umri wa miaka 27, kwenye orodha yao ya kipaumbele kuchukua nafasi ya kiungo wa kati wa England, Declan Rice, iwapo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ataondoka msimu wa majira ya joto. ***(Sun)***

### ALVAREZ, CITY WATETA

KLABU ya Manchester City inapanga kufanya mazungumzo na mshindi wa Kombe la Dunia na Argentina, Julian Alvarez, kuhusu mkataba mpya, licha ya mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 23, kuwasili Etihad msimu uliopita wa majira ya joto. ***(Mirror)***

### SPURS NAYO KUNUNULIWA

WAWEKEZAJI wa Qatar wanaweza kutoa ofa ya kununua hisa Tottenham, hata kama Sheikh Jassim Bin Hamad Al Thani atakamilisha kuinunua Manchester United. ***(Times)***

### ROBINSON AWINDWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inapanga kumnunua beki wa pembeni wa Fulham na Marekani, Antonee Robinson mwenye umri wa miaka 25. ***(Football Insider)***

### FELIX CHUPUCHUPU BARCA

BARCELONA ilikubali kumsajili mshambuliaji wa Atletico Madrid na Ureno, Joao Felix, Januari 2022, lakini dili hilo lilikwama kwa sababu ya kanuni za haki sawa za kifedha. ***(AS)***

### O'BRIEN AVUTIA MAREKANI

KIUNGO wa kati wa Nottingham Forest, Lewis O'Brien, mwenye umri wa miaka 24, anazivutia klabu za Ligi ya Marekani za New York City, Columbus Crew na Atlanta United. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL INAWEZA KUFIKIA KILA KITU EPL - ZINCHENKO

Kutokana na mchezo huo, tumechukua somo la kushangaza kwetu sote ambalo tunahitaji kuwa nalo hadi mwisho...

**LONDON, England**

OLEKSANDR Zinchenko amesisitiza kuwa Arsenal inaweza kufikia "kila kitu inachotaka" baada ya kikosi hicho cha Mikel Arteta kutoka nyuma mara mbili na kuifunga Aston Villa na kufufua matumaini yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England.

'Washikabunduki' hao walifunga mabao mawili dakika za lala salama na kurejea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu hivyo kumaliza mfululizo wa mechi tatu bila ushindi baada ya kushinda mabao 4-2 Jumamosi.

Ollie Watkins aliipatia Villa bao la kuongoza la mapema naye Philippe Coutinho, akianza kwa mara ya kwanza Ligi Kuu England chini ya kocha wa zamani wa Arsenal, Unai Emery, akaongeza la pili baada ya Bukayo Saka kusawazisha.

Zinchenko kisha akarejesha usawa, kabla ya mabao mawili dakika za lala salama - bao la kujifunga kutoka kwa Emi Martinez baada ya shuti la Jorginho kugonga mwamba na kisha kumgonga yeye na Gabriel Martinelli akafunga la nne.

"Kutokana na mchezo huo ningependa kusema mambo mawili," alisema Zinchenko akiiambia BT Sport.

"Kwanza, tulichukua somo la kushangaza kwetu sote ambalo tunahitaji kuwa nalo hadi mwisho.

"Kama nilivyosema siku za nyuma, kikundi hiki kina watu wa ajabu sana, wanaweza kufikia kila kitu wanachotaka ikiwa tutaendelea kupigana na kuendelea kujiamini. Mwitikio kutoka kwetu sote katika kipindi cha pili ni njia nzuri ya kwenda.

"Tungependa kuingia kwenye chumba cha kubadilishia nguo haraka iwezekanavyo, lakini bado kuna michezo mingi ya kucheza na tunahitaji tu kuendelea, kupambana na kuendelea kuamini tunaweza kufanya kila kitu."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 481,
MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13


PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ANCELOTTI: HUYU VINICIUS NI MCHEZAJI WA KIPEKEE



**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti alimsifu Vinicius Junior kama "mchezaji wa kipekee" baada ya nyota huyo wa Real Madrid kuiongoza timu hiyo bila ya Karim Benzema.

Mfungaji bora wa LaLiga wa Madrid, Benzema alipumzishwa kwenye mchezo huo wa Jumamosi dhidi ya Osasuna kwa ajili ya mechi ya kesho Jumanne ya hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool.

Vinicius alifunga mara mbili, lakini mabao yote yalikataliwa kwa kuotea pale kwenye dimba la El Sadar na akasaidia bao la Federico Valverde wakati Madrid ikishinda 2-0 na kupunguza uongozi wa Barcelona kwenye kilele cha Ligi Kuu Hispania hadi alama tano.

Winga huyo wa Brazil alitengeneza nafasi tatu kwa 'Los Blancos' hao, jambo ambalo lilimfurahisha kocha Ancelotti.

"Ni wazi kwamba Vinicius ni mchezaji anayeleta mabadiliko," alisema Muitaliano huyo katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Alicheza mchezo mzuri. Ni mwanasoka wa ajabu."

Kikosi hicho cha Ancelotti kililazimika kusubiri hadi kipindi cha pili ili kuweza kupata mabao hayo ambapo dakika ya 78 Valverde alifunga la kwanza kabla ya Marco Asensio kufunga la pili dakika 14 baadaye.

"Nilichopenda zaidi ni kwamba tumefanya katika kipindi cha pili kile ambacho tungeweza kufanya katika kipindi cha kwanza," aliongeza.

"Nilichopenda zaidi ni kwamba timu haijapoteza akili na imekuwa vumilivu katika hatua za mwisho. Timu imecheza vizuri. Imelazimika kuteseka ilipolazimika kuteseka na tumeridhika sana na hilo."

Toni Kroos pia alikosa mchezo huo pamoja na Aurelien Tcouhameni, lakini Ancelotti aliwahakikishia Madrid watakuwa tayari kwa mechi ya kwanza ya 16-bora ya Ligi ya mabingwa Ulaya pale Anfield.

"Tulikuwa na tatizo la dakika za mwisho na Tchoaumeni, lakini tuko sawa," aliendelea.

"Tutaingia kwenye mchezo wa Jumanne tukiwa na mienendo mizuri. Wachezaji wanaendelea na ahueni na tutafika tukiwa na imani."

# Nunez pigo Liverpool kuelekea Uefa

**LIVERPOOL, England**


DARWIN Nunez atafanyiwa vipimo vya jeraha la bega ambalo limemfanya fowadi huyo wa Liverpool kuwa na shaka kwa mechi ya Jumanne ya hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid kwenye Uwanja wa Anfield.

Nunez mwenye umri wa miaka 23, alifunga bao lake la kwanza la Ligi Kuu England tangu kabla ya Kombe la Dunia na kuwaweka Liverpool kwenye njia ya ushindi wa 2-0 dhidi ya Newcastle Uwanja wa St James' Park Jumamosi, ushindi ambao unaifanya timu ya Jurgen Klopp kupanda hadi nafasi ya nane, pointi sita nyuma ya Newcastle walio katika nafasi ya nne wakiwa na mchezo mkononi.

Lakini mchezaji aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 75 kutoka Benfica, alitolewa dakika 59 na nafasi yake kuchukuliwa na Roberto Firmino, baada ya kupata jeraha la bega.

Na baada ya ushindi huo, kocha wa Liverpool, Klopp alisema kuwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay anahitaji kufanyiwa tathmini zaidi ili kugundua ukubwa kamili wa jeraha hilo.

"Nunez ameumia bega na anahitaji tathmini zaidi," alisema Klopp. "Hatujui zaidi kwa sasa, itabidi tuone."



# HABARI MICHEZO


# 755,620 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 21/02/23 | 22:45 | Rotherham vs Sunderland | 3.12 | 3.32 | 2.18 |
| 02. 21/02/23 | 22:45 | Swansea vs Stoke City | 2.20 | 3.22 | 3.17 |
| 03. 21/02/23 | 22:45 | Millwall vs Burnley | 2.88 | 3.22 | 2.37 |
| 04. 21/02/23 | 23:00 | Liverpool vs Real Madrid | 2.29 | 3.47 | 2.82 |
| 05. 22/02/23 | 02:05 | Tlaxcala FC vs CD Tapatio | 2.37 | 3.20 | 2.74 |
| 06. 23/02/23 | 17:00 | Bengaluru FC vs FC Goa | 2.39 | 3.47 | 2.54 |
| 07. 23/02/23 | 20:45 | SC Dnipro 1 vs AEK Larnaca | 2.22 | 3.30 | 3.15 |
| 08. 23/02/23 | 20:45 | PSV Eindhoven vs Sevilla FC | 2.21 | 3.50 | 3.00 |
| 09. 23/02/23 | 20:45 | Monaco vs Bayer Leverkusen | 2.22 | 3.50 | 3.00 |
| 10. 23/02/23 | 23:00 | FC Basel vs Trabzonspor | 2.30 | 3.39 | 2.94 |
| 11. 23/02/23 | 23:00 | Union Berlin vs Ajax | 2.25 | 3.19 | 3.19 |
| 12. 23/02/23 | 23:00 | Manchester Utd vs Barcelona | 2.38 | 3.26 | 2.92 |
| 13. 24/02/23 | 19:00 | HNK Sibenik vs Istra | 2.90 | 2.90 | 2.44 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 20/02/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 4022 | Havadar vs MES Rafsanjan | 2.20 | 2.76 | 3.54 |
| 16:00 | 2032 | AL Khlood vs AL Hazm | 3.75 | 2.80 | 1.93 |
| 16:00 | 3581 | Crewe U23 vs Hull City U23 | 4.10 | 4.00 | 1.65 |
| 16:20 | 4093 | Ohud Medina vs Al Ahli Jeddah | 4.04 | 2.95 | 1.95 |
| 16:30 | 3579 | Roma Youth vs Atalanta Youth | 1.53 | 4.24 | 4.75 |
| 16:30 | 3983 | Neroca FC vs Minerva FC | 3.48 | 3.17 | 2.01 |
| 16:45 | 3212 | Al Gharafa SC vs Al-Shamal | 1.53 | 4.26 | 4.77 |
| 16:50 | 1453 | AL Tadamon vs Al Fehaheel | 2.94 | 3.25 | 2.21 |
| 18:00 | 3795 | Botosani vs Sepsi Osk | 3.75 | 3.22 | 1.99 |
| 18:00 | 5521 | El Daklyeh vs El Ittihad Alexandria | 3.64 | 2.94 | 2.17 |
| 18:30 | 4819 | Busaiteen vs Etehad Alreef | 1.37 | 4.44 | 6.82 |
| 18:30 | 5343 | Juventus Youth vs Empoli Youth | 1.85 | 3.63 | 3.53 |
| 18:30 | 5404 | ISA Town vs Aali | 2.75 | 3.06 | 2.45 |
| 18:30 | 5559 | Najma Manama vs Al-Tadamun Buri | 1.13 | 6.00 | 12.00 |
| 18:50 | 5372 | Najran SC vs AL Riyadh | 3.99 | 3.00 | 1.94 |
| 19:00 | 1714 | Atromitos vs Levadiakos | 1.85 | 3.17 | 4.55 |
| 19:20 | 4993 | AL Arabi vs AL Sahel | 1.62 | 3.64 | 4.78 |
| 20:00 | 1667 | Maccabi Petach Tikva vs Hapoel Kfar Saba | 1.79 | 3.25 | 3.60 |
| 20:00 | 2875 | Sandecja vs Resovia Rzeszow | 2.07 | 3.22 | 3.27 |
| 20:00 | 3845 | Anorthosis Famagusta vs Pafos FC | 3.19 | 3.30 | 2.20 |
| 20:00 | 4566 | Ahi Nazareth vs El Fahem | 3.36 | 3.09 | 2.23 |
| 20:00 | 4803 | AS Ashdod vs Bnei Yehuda | 3.99 | 3.36 | 1.92 |
| 20:00 | 5119 | Olympiakos Nicosia vs Omonia Nicosia | 4.37 | 3.68 | 1.76 |
| 20:00 | 5654 | Enppi Club vs Talaea El Gaish | 2.65 | 2.90 | 2.90 |
| 20:30 | 2129 | Brommapojkarna vs Orebro SK | 1.66 | 3.79 | 4.26 |
| 20:30 | 3335 | Djurgardens IF vs Landskrona Bois | 1.21 | 5.80 | 9.74 |
| 20:30 | 3745 | IFK Goteborg vs Utsiktens BK | 1.49 | 4.09 | 5.39 |
| 20:30 | 4901 | OFI Crete vs Aris Salonica | 2.81 | 3.12 | 2.51 |
| 21:00 | 1162 | Lommel U21 vs RWD Molenbeek U21 | 2.24 | 3.37 | 2.80 |
| 21:00 | 2268 | Radomiak Radom vs Jagiellonia | 2.03 | 3.17 | 3.43 |
| 21:00 | 2619 | VfB Oldenburg vs Hallescher | 2.80 | 3.32 | 2.37 |
| 21:00 | 3013 | Viborg FF vs Midtjylland | 2.36 | 3.23 | 2.93 |
| 21:00 | 3483 | Al Hilal Riyadh vs Shabab AL Ahli Dubai Club | 1.57 | 3.95 | 4.78 |
| 21:00 | 4544 | U Craiova SA vs Voluntari | 1.98 | 3.17 | 3.86 |
| 21:00 | 4616 | Diosgyori Vtk vs Pecs MFC | 1.77 | 3.47 | 4.04 |
| 21:30 | 2035 | Maccabi Tel Aviv vs Hapoel Beer Sheva | 1.89 | 3.33 | 3.69 |
| 22:00 | 1048 | Jong Ajax vs Maastricht | 1.90 | 3.95 | 3.26 |
| 22:00 | 2051 | Jong Utrecht vs NAC Breda | 2.53 | 3.41 | 2.52 |
| 22:00 | 2221 | GD Chaves vs Sporting Lisbon | 6.36 | 4.47 | 1.44 |
| 22:00 | 3061 | FCV Dender EH U21 vs Lierse SK U21 | 2.90 | 3.48 | 2.14 |
| 22:00 | 4988 | Westerlo U21 vs St Truiden U21 | 5.41 | 4.58 | 1.44 |
| 22:30 | 5910 | Cesena vs AC Reggiana | 2.33 | 3.10 | 3.15 |
| 22:45 | 3697 | Bradford PA vs Blyth Spartans | 2.15 | 3.23 | 3.07 |
| 22:45 | 4028 | Nimes vs St Etienne | 3.31 | 3.31 | 2.10 |
| 22:45 | 4500 | Torino vs Cremonese | 1.64 | 3.61 | 5.15 |
| 22:45 | 4915 | Chelmsford vs Tonbridge Angels | 2.07 | 3.32 | 3.16 |
| 23:00 | 1934 | Malaga vs Zaragoza | 2.54 | 2.89 | 2.94 |
| 23:00 | 2443 | FC Martigues vs Villefranche Sur Saone | 2.32 | 3.14 | 2.99 |
| 23:00 | 3895 | Watford vs West Bromwich | 2.62 | 3.22 | 2.58 |
| 23:00 | 5166 | Getafe vs Valencia | 2.75 | 2.80 | 2.85 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KAGERA YAONA MWEZI BAADA YA MECHI NANE

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Kagera Sugar imezika mzimu wa kutopata ushindi kwa mechi saba mfululizo baada ya juzi kuifunga Namungo FC bao 1-0 kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

Ushindi huo umeipandisha timu hiyo hadi nafasi ya sita ya msimamo wa Ligi Kuu, sasa ikiwa na pointi 29 kwa mechi 23 ilizocheza.

Lilikuwa ni bao la Erick Mwijage akimalizia kazi nzuri iliyofanywa na Dickson Mhilu dakika ya 79, iliyohitimisha ukame wa ushindi wa timu hiyo.

Kabla ya mechi ya juzi, mara ya mwisho kwa timu hiyo kushinda ilikuwa ni Desemba 2, mwaka jana ilipoifunga Ihefu mabao 2-0 kwenye uwanja huo huo wa nyumbani.

Baada ya mechi hiyo, ikatoa sare mechi tano na kupoteza mbili.

Ilichapwa mabao 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji na bao 1-0 dhidi ya Singida Big Stars, suluhu dhidi ya Polisi Tanzania na Coastal Union, sare ya mabao 2-2 dhidi ya Geita Gold na Azam FC, sare ya bao 1-1 dhidi ya Simba.

"Ligi ni ngumu sana, kila timu kwa sasa inapambana ili kujinasua, kuna zingine zinapambana kupata ubingwa, lakini zipo zinazopambana ili zisishuke daraja, kikubwa ni kwamba ukishinda wachezaji wanapata moyo na ari ya kujiamini, mimi kama kocha ninachojaribu ni kupunguza makosa ambayo yanajitokeza kwenye mechi mbalimbali zilizopita," alisema Mecky Mexime Kocha Mkuu wa timu hiyo.

Wakati Kagera Sugar ikipanda hadi nafasi ya sita, Namungo imerudi kwenye nafasi ya saba, ikiwa na pointi hizo hizo 29, timu hizo zikiachana kwa mabao ya kufunga na kufungwa. Kagera Sugar imefunga mabao 21, Namungo ikiwa na mabao 19.




Mshambuliaji wa Arsenal, Gabriel Martinelli, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la nne wakati ikishinda 4-2 dhidi ya Aston Villa kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Villa Park juzi na kuiwezesha timu yake kurejea kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA MATARAJIO CAF SASA HESABU ZA VIDOLE

INATOKA UK. 24

itakuwa imefikisha pointi 12, wakati mabingwa hao wa Guinea watabaki na alama zao nne kabla ya kufunga hatua ya makundi dhidi ya Vipers.

Hivyo, hata kama Horoya itashinda dhidi ya Vipers na kutoka sare mechi moja dhidi ya Raja Casablanca ina maana itamaliza na pointi nane, moja nyuma ya Simba ambayo haipewi nafasi kubwa ya kwenda kuambulia hata sare ugenini dhidi ya miamba hiyo ya Morocco.

Akizungumzia mchezo huo wa juzi dhidi ya Raja Casablanca, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, alisema uzoefu na ubora wa kikosi cha wapinzani wao, ndicho kilichowagaribu katika mchezo huo wa pili wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Robertinho alisema wachezaji wake walicheza vizuri, lakini walipaswa kufanya zaidi ya walichofanya kwa sababu ya ubora na uzoefu mkubwa wa Raja Casablanca.

"Kipindi cha pili tulitulia tukafanya mambo kwa usahihi, ila bado haikutosha, lakini huu ni mpira na matokeo haya si ya kushangaza badala yake tunajiandaa na mchezo ujao wa ugenini dhidi ya Vipers wikiendi ijayo," alisema Robertinho.

Alisema nyota wake wawili, Jean Baleke na Saido Ntibanzokiza hawakuwa fiti kwa asilimia kubwa kwa sababu ya kutoka katika majeraha.

Robertinho alisema matokeo ya juzi wanapaswa kuyasahau na kujiandaa na mchezo ujao wa ugenini dhidi ya Vipers ya Uganda, kwa kufanya maandalizi mazuri ili kupata matokeo chanya.

"Bado tuna mechi nyingine mbele, ni vizuri kujipanga kuliko kusononeka na matokeo haya, kuma michezo mingine iliyopo mbele yetu kujiandaa kwa kufanyia kazi madhaifu yote yaliyojitokeza katika mchezo wa leo (juzi)," alisema Robertinho.

Naye Kocha Mkuu wa Raja Casablanca, Modher Keboir, alisema kabla ya kucheza mchezo huo alitumia muda mwingi kuwasoma Simba katika michezo mbalimbali na kufanikiwa katika mbinu zake.

Alisema anatambua ugumu wa kuifunga Simba nyumbani kwao na amefanikiwa katika mipango aliyoingia nayo kwa kucheza kwa uzoefu mkubwa na kushinda kwa mabao 3-0.

"Simba ni timu nzuri na ngumu kuwafunga katika uwanja wa nyumbani kwao, nimefanikiwa katika mbinu zetu baada ya kuwasoma wapinzani wetu vizuri," alisema Keboir.

Simba itasafiri kwenda kuivaa Vipers nchini Uganda Jumamosi wiki hii wakati Raja Casablanca itakuwa nyumbani kuikaribisha Horoya AC.

# Michezo

Jumatatu Februari 20, 2023
Nipashe



UKURASA 21

**Arsenal inaweza kufikia kila kitu EPL - Zinchenko**

**DALUGA...**



Mshambuliaji wa Simba, John Bocco, akiruka daluga la kiungo mkabaji wa Raja Casablanca ya Morocco, Roger Aholou, kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na kumalizika kwa wenyeji kukubali kichapo cha mabao 3-0. **MPIGAPICHA WETU**

# Simba matarajio CAF sasa hesabu za vidole

●●●Kocha Raja Casablanca atoa sababu kushinda, Robertinho naye afunguka asema sasa sahauni...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukubali kichapo cha pili kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wawakilishi wa Tanzania, Klabu ya Simba, sasa matarajio yao pekee ya kutinga robo fainali ya michuano hiyo ni kwa kutegemea hesabu za vidole.

Simba ambayo imekuwa na rekodi nzuri ya ushindi inapocheza katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, juzi ilikubali kichapo cha mabao 3-0 uwanjani hapo dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco, hicho kikiwa kipigo cha pili katika hatua hiyo baada ya mechi ya awali ugenini nchini Guinea kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Horoya AC.

Lakini kipigo hicho katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa Simba ni cha kwanza kwao katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kufungwa uwanjani hapo katika ushiriki wake wote wa michuano hiyo.

Matokeo hayo yanaifanya Raja Casablanca kuongoza Kundi C kwa kuwa na pointi sita, ikifuatiwa na Horoya AC yenye alama nne na Vipers ya Uganda ikishika nafasi ya tatu kwa pointi yake moja huku Simba ikiburuza mkia bila pointi yoyote.

Kwa maana hiyo, ili Simba iweze kutinga hatua ya robo fainali sasa inatabidi kutegemea hesabu za vidole, kwanza inapaswa kushinda michezo yake mitatu ijayo dhidi ya Vipers ugenini na nyumbani na kisha itapaoikaribisha Horoya AC hapa nchini, lakini kuiombea mema Raja Casablaca ishinde michezo yake mitatu ijayo kabla ya kuhitimisha kwa kukutana na Wekundu wa Msimbazi hao.

Hii ina maana kama Simba ikishinda mechi zake tatu kabla ya kuhitimisha dhidi ya Raja Casablaca, itafikisha pointi tisa, huku mimba hiyo ya Morocco ikishinda tu dhidi ya Horoya nyumbani na ugenini,

INAENDELEA UK. 23

## Yanga, Azam zaivuruga KMC

**Na Hadija Mngwai**

TIMU ya KMC imejikuta katika wakati mgumu kutokana na kuwa na mechi ngumu mfululizo dhidi ya Yanga na Azam huku ikiwa katika nafasi ya 12 ya msimamo wa Ligi Kuu Bara.

KMC ambayo ipo nafasi ya 12 ikiwa na alama 23, Jumatano inatarajia kuvaana na Yanga huku Jumamosi wiki hii ikishuka dimbani dhidi ya Azam FC ambayo na yenyewe inawania angalau kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa KMC, Christina Mwagala, amesema kipindi walichonacho kwa sasa ni kigumu kutokana na kukabiliwa na michezo migumu dhidi ya Yanga na Azam zote zikiwa zinawania nafasi za juu.

"Mechi yetu na Yanga itakuwa ngumu kwa kuwa wao wapo katika presha ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa, pia wanaongoza kwenye msimamo, hivyo wanahitaji kupata matokeo mazuri.

"Pia ukiangalia wamepishana pointi sita na wapinzani wao, Simba hivyo, watahitaji ushindi ili wasipoteze pointi kwa kupata alama tatu," alisema na kuongeza:

"Ukiangalia katika kipindi hiki, KMC inapitia wakati mgumu zaidi ya vipindi vyote kwani Jumatano tunacheza na Yanga kisha Jumamosi tunacheza na Azam ambayo inahitaji kujiweka vizuri, mechi zote ngumu huku tukiwa nafasi ya 12.

"Ukiachana na michezo hiyo wanaotufuatia nyuma wanapambana ili na wao waweze kuja juu, lakini tumejipanga kufanya vizuri na hali ya kikosi ipo vizuri wachezaji wetu ambao walikuwa majeruhi wamerejea kwa ajili ya kupambana ili kumaliza katika nafasi nzuri," alisema Mwagala.

Yanga ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 59, ikifuatiwa na Simba yenye pointi 53, zote zikiwa zimecheza mechi 22, huku Singida Big Stars iliyopo nafasi ya tatu yenyewe na alama 44 ilizozipata kwa kushuka dimbani mara 23.

Azam FC iliyoshuka dimbani mara 22, yenyewe ipo nafasi ya nne ikiwa na pointi 43, jambo ambalo linaongeza ushindani kati yao na Singida Big Stars kuwania kumaliza nafasi ya tatu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >